

DHIHAKA KWA SABABU YA NENO



Asante, Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Amina."—Mh.]

Nilimwambia Ndugu Neville, "Una hakika huna kabisa upako mdogo asubuhi ya leo?"

² Mimi nilishuka kuja kuwaombea wagonjwa. Kulikuwako na watu waliokusanyika katika kile tunachoninii...mapema Jumapili asubuhi. Wale ninaoweza kuwapata pale, ninawafanya tu waje hapa kanisani. Na mimi—mimi daima nafikiri ni vyema kuwaombea wagonjwa kwenye kanisa. Sijui. Ninapenda kanisa, na kushuka kuja hapa ambapo kusanyiko, watu wako huku wakiomba.

³ Na kulikuwako na msichana mdogo kule nyuma, msichana mdogo aliye mrembo sana, mbona, nafikiri ameketi mahali fulani hapa sasa, kama hao watu hawakuenda nyumbani. Loo, naona sasa. Na huyo ndiye aliye mrembo kuzidi watoto wote. Naye ni mgonjwa sana. Nasi tulikuwa tukisikiliza, tuliposikia ujumbe wa lugha na fasiri ikitolewa. Nasi tulikuwa tukisikiliza, na tulifikiri tulielewa kwamba kitu fulani kilisemwa kuhusu msichana mdogo. Na tulikuwa tuingojea kuona kama Bwana alitoa ujumbe, jambo la kusema katika hilo. Lakini nafikiri maskini msichana huyo ni mzima sasa, na atapata afya. Na kwa hiyo...

⁴ Na kulikuwa na mama aliyekuwa kipofu, pia, na tulikuwa tukimwombea. Na mtu fulani kwenye ambalanzi huko nje, mhudumu. Sidhani mtu huyo angelikuwa na uzito wa ratili thelathini na tano, ama arobaini. Ninii—ninii tu, sana... Na kwa hiyo nikashuka nikaja kuwaombea.

⁵ Na sababu ya mimi kusitasita kwa namna fulani, sana, kijazo kilidondoka kutoka kwenye jino langu. Nami ninajipigia mbinja, asubuhi ya leo, kutokea mahali hapo kutoka kwenye jino langu pale, pale mbele. Na wananiambia sasa sina budi kuyapeleka yakasagwe, na yawekewe vifuniko. Na kwa hiyo uzee huu unanyemelea tu, ndilo jambo tu nijualo. Na nilikuwa na kijazo kwenye hilo, na kwa namna fulani nusu yake, na nilipoanza kuzungumza, unaweza kulihisi, upepo kwa namna fulani unasukumia nje, mwa—mwajua ninalomaanisha, inatokea midomoni mwako. Na kwa namna fulani inakufanya kupiga kitembe, kitu kama hicho.

⁶ Kwa kweli sisi ni watu waliopendelewa kuwa hai asubuhi ya leo, na kuweza kuja kanisani. Na kwenye mkesho huu wa Krismasi, tuingojea sherehe waliyo nayo, ambayo, na—natumaini mimi...Kuna watoto wengi kupita kiasi hapa asubuhi ya leo, kwa hiyo nitatulia tu. Unaona? Na sisi watu

wazima, wakati mwingine, tunazungumza mambo ambayo watoto wadogo hawapaswi hata kuyasikia, mwajua.

⁷ Lakini, nadhani kanisa lina zawadi ndogo hapa kwa ajili ya watoto wadogo, baada ya kitambo kidogo. Nilikuwa tu nikiiangalia, huko nyuma. Loo, mnataka kubaki. Baada ya shule ya Jumapili, ngojeeni tu, mnaona, kwa maana na—nafikiri wana zawadi huko nyuma kwa ajili ya watoto wadogo, za kuwapa asubuhi ya leo. Na wakati ninaponinii. . . Enyi watoto wadogo, kumbukeni, wakati tukifanya jambo hili, ninataka kuweka jambo hili dhahiri, si Baba Krismasi, kwa maana hiyo ni hadithi ambayo siku moja mtajua haina maana. Lakini ni kutoka kwa Yesu Kristo, Kweli ya kweli zote, mnaona, Mwana wa Mungu. Nasi tunawapa zawadi hii ndogo, asubuhi ya leo, kwa sababu ni kuwafanya mjue ya kwamba wakati mmoja Mungu alitoa zawaidi iliyo kuu sana ambayo ingeliweza kupewa jamii ya wanadamu: Mwanawe. Nasi tuna njia mbaya, kuelezea. Wala hakuna kitu tunachoweza kutoa cha kulinganisha nayo. Lakini kama binadamu tu, mmoja kwa mwingine, tunafanya hivyo.

⁸ Sasa, nilikuwa nikitaka kungojea hadi Jumapili ijayo. Na labda nitangojea, kwa vyovyote vile, juu ya kitu nilichotaka kusema. Nasi tu—tumejulishwa jambo fulani, huko nyumbani, kuhusu ono, ambalo sina budi kulifuatilia. Na kwa namna fulani ni ninii. . . Kwa namna fulani, inaonekana, lingekuwa ni chungu, bali kamwe hatutaki kuwazia kwamba kile Mungu asemacho ni kichungu. Mizigo Ya—Yake ni myepesi.

⁹ Na kwa kuwa Jumapili ijayo, Mungu akipenda, tutakuwa na i—ibada hapa ambayo ni kabla tu ya Mkeshwa wa Mwaka Mpya, ikiwa Bwana atapendezwa nasi kuwa na ibada hii. Nasi tunataka kuwa na ibada ya asubuhi, maombi kwa ajili ya wagonjwa, na labda ibada ya ubatizo. Halafu niliwazia, tuitangaze kwa marafiki zetu, kwamba wangepewe kuja. Basi tutakuwa na Jumapili asubuhi na Jumapili usiku. Na kisha watu wanaotaka kubaki kwa ajili ya ya Mwaka Mpya, basi tutakuwa na. . . Je! tutakuwa na Mkeshwa, wakati huu? [Ndugu Neville anasema, “Ndiyo.”—Mh.]

¹⁰ Kutakuwako na wahudumu kadhaa hapa, watakaokuwa wakihubiri kwenye usiku wa Mwaka Mpya, mpaka usiku wa manane. Na—na sisi tunawaalika wahudumu kama hao waje wahubiri. Bwana akipenda, ninataka kuwa mmoja wao aliye na jambo la kuhubiri kwenye usiku wa Mwaka Mpya.

¹¹ Na halafu Jumapili ijayo, niliwazia ningeleta mlolongo wa mambo yanayofanywa, ambayo yamefanywa, kuonyesha jinsi Mungu anavyoshughulika na watu Wake, na kuyaleta moja kwa moja hadi kufikia kwenye ki—kilele hapa kanisani.

¹² Na wengi wenu mnashangaa kuhusu jambo hili la kodi ya mapato ambalo tumekuwa tukishughulikia. Limetatuliwa. Na kwa hiyo ninataka kuwaambia jinsi hilo lilivyotukia, pia.

Na ninafikiri, ingekuwa, kulazimika kulisimulia tena, Jumapili ijayo, kwa hiyo nitangojea tu mpaka Jumapili ijayo. Na kujaribu kuwazungumzia kidogo, asubuhi ya leo, kutoka kwenye Neno. Mnaona? Na Jumapili ijayo, nita—nitajaribu, Mungu akipenda, kuwaambia jinsi jambo lote lilivyotukia, na kuwaitea kila moja ya mambo ambayo Bwana alisema, na myaone yakitimia kikamilifu kabisa, yamewekwa mahali pao hasa. Mnaona? Yeye kamwe hasemi uongo.

¹³ Lakini, sasa, jambo moja ninalotaka kusema asubuhi ya leo, ambalo labda sitalisema, sitalisema Jumapili ijayo, ni kuhusu jambo fulani ambalo lilitukia jana. Kidogo nilikuwa sitaki kuja asubuhi ya leo, kwa sababu kwa kweli kidogo nimefadhaika, hivi kwamba kabisa si—sijisikii vizuri. Ila kwa kuwa nipo hapa, vema, nitajaribu vizuri niwezavyo.

¹⁴ Usiku uliotangulia wa jana, nilikuwa na wageni, Ndugu na Dada Sothmann, tunavyojua hapa, mmoja wa wadhamini wa kanisa, pamoja na mkewe, walikuja kututembelea mimi na mke wangu. Nasi tulikuwa tukizungumza juu ya mikutano ijayo huko Phoenix na sehemu zinazopazunguka, kama yakiwa ni mapenzi ya Bwana. Na tulikuwa macho mpaka karibu saa nne na nusu, nadhani, nami nikaenda kulala wakati fulani karibu na saa tano.

¹⁵ Na wakati fulani usiku, niliota ndoto. Na katika ndoto hii niliona mtu aliyedhaniwa kuwa ni baba yangu; mtu mkubwa, mkubwa mno, akiwakilisha tu, tukinena kwa mfano, baba yangu. Nilimwona mwanamke, hakuonekana kama mama yangu; lakini, hata hivyo, alidhaniwa kuwa ni mama yangu. Na mtu huyu (aliyedhaniwa kuwa kama ni baba, mume wa mwanamke huyu) alikuwa akimtesa kikatili, kwa jinsi kwamba alikuwa na kipande kikubwa cha mbao, naye angemnyanyua juu namna *hii* na kumtwanga kwa kipande hiki cha mbao, naye angelegea na kuanguka chini. Na kisha—na kisha, baada ya kitambo kidogo, angeamka tena. Naye angetembea huku na huku, akitaka kumtwanga tena, angemtanga tena. Nami nilikuwa nimesimama kwa mbali, nikiangalia.

¹⁶ Hatimaye, nikachoshwa kabisa na jambo hilo. Nami nilikuwa mdogo zaidi sana kuliko mtu huyu, aliyedhaniwa ni kama baba yangu. Kwa hiyo nikasogea karibu naye na kukitia kidole changu usoni mwake. Nikasema, “Usimtwange tena.” Unaona? Na nilipofanya hivyo, jambo fulani likianza kutukia. Mikono yangu ikaanza kudundadunda, nami nikapata misuli mikubwa mno, migumu mno. Sijapata kuona misuli kama hiyo. Nami nikamshika tu mtu huyo kwenye ukosi, na kusema, “Usimpige tena. Ukifanya hivyo, itakubidi kukabiliana nami kama ukimpiga tena.” Ndipo mtu huyo akaniogopa, na akamwacha. Nikaamka.

¹⁷ Vema, nikilala pale, katika dakika moja, naam, fasiri ya hiyo ikaja. Hiyo ilikuwa, hakuna budi, mwanamke huyo, kwa mfano, ni Kanisa, ambalo kwa namna fulani ni huyo mama. Huyo baba ni dhehebu lililo juu yake, linalolitawala Kanisa, kama vile mume alivyo mtawala wa mke. Na ni haya madhehebu yanayolipiga Kanisa hilo, wala hayaliachi lisimame kwa miguu Yake namna hiyo. Ninii tu, kila linapojaribu kusimama ama kufanya jambo fulani, hao, watu waliomo mle ndani, dhehebu linalipiga linaliangusha. Na inamaanisha tu kuweka misuli fu—fulani ya imani hapa nje kuendelea kuchomeka kidole changu huko nje, na kusema, “Unakabiliana nami. Unaona?” Maana, wapo watu mle ndani ambao ni wa Mungu. Na hiyo ilikuwa ni sawa. Yapata...

¹⁸ Tulikuwa tumeamka kwa karibu saa mbili, ama tatu, nadhani. Na binti yangu, mmoja wao, Rebekah, huko nyuma, yeye anafanya kazi kwenye Hospitali ya Methodisti huko Louisville. Ni, loo, ni nesi mwanafunzi. Ni “mfanya kazi wa kujitolea hospitalini,” ndivyo wanavyowaita, ama kitu kama hicho. Naye alikuwa, yeye... Walimwita aje huku asubuhi hiyo, na hilo ndilo lililoniambia. Na ilikuwa ni mapema, naye, pamoja na maskini mwenzake wa shuleni hapa, wana—wanafanya kazi kule pamoja, na nilikuwa niwapeleke Louisville. Ilibidi wawe huko saa nne. Na mke wangu akashangaa ni kwa nini asingeweza kuingia kwenye chumba cha kulala. Nilikuwa nimekifunga.

¹⁹ Sasa, nimekuwa na mambo mengi kutukia maishani mwangu, bali kamwe sijapata jambo lolote kama hilo. Nilipata njozi. Sijui tafsiri yake. Sijapata jambo kama hilo maishani mwangu. Lakini, mbele yangu, inaonekana ya kwamba nilitambua lilikuwa ni ono, nami nilikuwa katika ono hilo. Lakini nilikuwa nikizungumza na mwanangu, Joseph. Ambaye, yeye hakuwa humo chumbani wakati huo. Bali kwa namna fulani, mara tu liliponijia, nilikuwa nikizungumza na Joseph.

²⁰ Nami ni—nikaangalia juu. Na kwa namna fulani katika umbo la piramidi ndege wadogo, wadogo sana, wenye urefu wa kitu kama nusu inchi, walikuwa wamesimama mbele yangu. Nao walikuwa, hapo juu, juu ya matawi, kulikuwa na... naweza kusema, watatu ama wanne. Halafu, la pili, tawi la pili lilikuwa labda na wanane ama kumi. Na la chini kabisa, lilikuwa na kumi na watano ama ishirini.

²¹ Nao walikuwa ni askari wadogo wa vita, kwa kuwa mabawa yao yalikuwa yamegogwagongwa, na ilionekana kana kwamba walikuwa wakijaribu kuzungumza na mimi, wakisema jambo fulani. Nami nilikuwa magharibi, yaonekana karibu na Tucson, Arizona. Nao hao ndege walikuwa wakiangalia Mashariki. Nami nilikuwa nikisikiliza kwa makini. Walikuwa wakijaribu kusema, ilionekana kana kwamba walikuwa wakijaribu kuniambia jambo fulani. Nao walikuwa na manyoya madogo, yote

yalikuwa yamegongwagongwa, na kadhalika. Walikuwa na alama dhahiri sana za vita. Ndipo, mara, ndege mmoja akaanza kupachukua mahali pa huyo mwingine, wakiruka namna *hiyo*. Nao, hao ndege wadogo wakaondoka mbio, wakiruka kuelekea mashariki.

²² Na basi walipoondoka, kutokana na hao akaja ndege mkubwa zaidi, walifanana zaidi na hua, wakiwa na mabawa yaliyochongoka. Na—na—nao wakaja katika kundi kubwa, na kasi, kwa kasi zaidi ya vile wale ndege wadogo walivyoruka, wakaelekea mashariki.

²³ Na ningali katika ninii yangu . . . dhamiri hizo mbili pamoja, nilijua nilikuwa nimesimama hapa, nami nilijua nilikuwa mahali pengine. Mnaona? Nami nikawaza, “Sasa, hili ni ono, nami sina budi kujua ni nini maana ya hili.”

²⁴ Na mara hilo kundi la pili la ndege lilipokuja hapo, niliangalia Magharibi. Na ilionekana kama katika umbo la piramidi, kama vile wawili kila upande, mmoja akiwa juu kileleni, wakaja watano wa Malaika wenye nguvu sana niliowahi kuona maishani mwangu. Mwendo wa kasi sana wa kutisha sijawahi kuona. Vichwa vyao vimeelekezwa nyuma na mabawa Yao yaliyochongoka, wakiruka tu haraka! Ndipo nguvu za Mwenyezi Mungu zikanishukia, kwa namna ambayo, mpaka ikaniinua kabisa toka ardhini, moja kwa moja toka ardhini, kwenda juu.

Niliweza kumsikia Joseph angali akinena.

²⁵ Na ilisikika kama ni mpasuko wa mapatano ya spidi ya ndege na ya sauti, huo—huo mngurumo mkubwa ukarindima, huko mbali sana, upande wa Kusini. Na wakati nilipoinuliwa . . . Na kulikuwako na mwendo wa kasi mno wa hao Malaika! Nami na—naweza tu kuwaona sasa hivi, mnaona, jinsi—jinsi Wao walivyokuwa wakija, katika lile umbo namna *hiyo*, wakija moja kwa moja kuingia kwangu.

²⁶ Sasa, sio kuota, sasa. La. Nilikuwa kabisa pale, nikiwa macho kabisa kama nilivyo sasa. Mnaona?

²⁷ Lakini hawa hapa wanakuja. Nao walikuja kasi mno, mpaka nikawazia, wakati ilipoinua juu . . . Nilisikia huo mlipuko, kitu kama hicho, ama kama mpasuko uliipasuka, kama mapatano ya spidi ya ndege na sauti. Na wakati ilipofanya hivyo, nikawazia, “Vema, hii haina budi inamaanisha ya kwamba niko karibu kuuawa, unaona, katika mlipuko wa namna fulani.” Ndipo—ndipo basi nikaninii tu . . . Wakati nikifikiri juu ya mambo hayo, nikawazia, “La, lisingekuwa hilo. Kwa kuwa, kama ulikuwa ni mlipuko, ungalimdhuru Joseph, pia. Maana, huyo hapo, angali anazungumza, akifikiri niko pale. Ninaweza kumsikia. Haukuwa huo.”

²⁸ Sasa, hili lote lingali ni kwenye ono. Halikuwa . . . Unaona? Lilikuwa katika ono.

²⁹ Ndipo basi, mara, nilipotambua ya kwamba nilikuwa... Walikuwa wamenizunguka. Nisingeweza kuwaona, bali nilikuwa nimeingizwa kwenye kundi hili Lao la piramidi, ndani ya kundi hili la—la Malaika, la watano. Nami nikawazia, “Sasa, Malaika wa mauti angekuwa ni mmoja. Watano wangekuwa ni neema.” Nilikuwa nikiwazia jambo hilo. Nikawazia, “Loo! Wana—wanakuja na Ujumbe wangu. Huo ndio upeo wangu wa pili. Wanakuja kuniletea Ujumbe kutoka kwa Bwana.” Basi nikapaza sauti kwa nguvu zangu zote, kwa sauti nilivyoweza, “Ee Yesu, ungetaka nifanye nini?” Ndipo nilipofanya hivyo, lilininii tu—liliniacha tu.

³⁰ Si—si—sijajisikia vema hata, tangu wakati huo. Mnaona? Nilikuwa, siku nzima jana, ilinibidi nikae nyumbani, karibu sijitambui. Siwezi kukituliza kichwa changu. Na utukufu na nguvu za Bwana! Nilipata ganzi mwili mzima, wakati liliponiacha. Nilikuwa nikijaribu kuisugua mikono yangu. Ndipo nikawazia, “Siwezi kupumua.” Ndipo nikatembea huku na huku, na sakafuni kote, na huku na huku. Nikawazia, “Hili lina maana gani, Bwana? Lina maana gani?” Ndipo, nikasimama. Nikasema, “Bwana Mungu, Mtumishi Wako ni... Si—siwezi kabisa kufahamu. Mbona? Hiyo ilikuwa ni nini? Jalia ijulikane, Bwana.” Vema, wakati ninii... .

³¹ Siwezi kuwaambieni kuhusu, wakati ninaposema, “Nguvu za Bwana.” Hakuna njia ya kuelezea jambo hilo. Si kile mnachohisi hapa, na baraka. Hizo ni baraka za Bwana. Hili ni takatifu! Loo, jamani! Ni—ni zaidi ya chochote ambacho mwanadamu angeweza hata kuwazia. Mnaona? Nalo—nalo lilikuwa likinisumbua, vibaya sana. Halininii... Si baraka. Ni usumbufu. Unasumbuka. Mnaona? Hivyo tu. Laiti mngalininii tu... .

³² Laiti ningalipata njia fulani ya kuwaambia watu kile hilo lilikuwa, ama kile ninii... jinsi nilivyojisia! Hilo, si kama tu kuketi hapa, mnataka kushangilia. Ni ninii—ni kitu fulani ambacho kila neva ndani yako inaninii tu... Ni zaidi ya tishio. Ni zaidi ya kutishwa. Ni kicho kitakatifu. Ya... mimi... Hakuna njia ya kulielezea. Hata, mpaka, mgongo wangu wote, juu na chini ya uti wangu wa mgongo, kupitia vidole vyangu, juu na chini ya miguu yangu na vidole, utu wangu wote ulishikwa tu na ganzi, mnaona, kama tu mtu uli—ulikuwa umetoka ulimwenguni, mahali fulani. Na—na zilikuwa zikiniacha, polepole, nami nikamwambia nanii—Bwana, “Je! utanijalia kujua, Ee Mungu?”

³³ Nadhani, ya kwamba, tukio la karibu sana la kuwa na nguvu hivyo tena, lilikuwa ni wakati nilipokuwa Zurich, Uswisi, ule wakati ambapo Yeye alinionesha yule Tai wa Kijerumani akimwangalia mpanda farasi wa Kiingereza akishuka kuja kupitia Afrika. Naye akasema, “Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu.”

³⁴ Nami nilikuwa nikimlilia Bwana, anisaidie. Nami—nataka anipe fasiri yake, kwa maana nilishangaa kama ilimaanisha—kama ilimaanisha ya kwamba nilikuwa nitaondoka, nilikuwa nitauawa. Na kama ilikuwa ndivyo hivyo, singeiambia familia yangu chochote juu yake. Ikiwa ni wakati wangu wa kwenda Nyumbani, mbona, nitaenda tu Nyumbani, hivyo tu. Lakini kama—kama hivyo ndivyo ilivyomaanisha, sikutaka kuiambia familia, sikuwataka wajue lolote kulihusu. Acha tu litendeke, na hilo—hilo lingekuwa hivyo tu.

³⁵ Nikasema, “Bwana, nisaidie. Sitaki kuiambia familia, kama—kama unaninii...Huu, ni wito wangu wa kwenda Nyumbani, vema, nita—nitakwenda, unaona,” nikasema. Na, wajua, unaninii... .

³⁶ Mnasema, “Vema, mbona hukuwazia juu ya yale uliyosema katika ono, kile ono lilichosema?”

³⁷ Lakini huwezi kuwazia juu ya mambo kama hayo wakati huo. Wewe...Siwezi, kwa vyovyote vile. Basi nikawaza... Nilikuwa tu nikitaabika, nimefadhaika. Hujui la kuwazia. Huwezi kuwazia.

³⁸ Nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, kama hilo lilimaanisha ya kwamba—ya kwamba mlipuko ulikuwa unaenda kunichukua, vema, jalia nijue sasa, ili kwamba nisiseme lolote juu yake. Jalia utukufu na nguvu Zako zije juu yangu tena, na ziniinue juu tena. Ataka, jalia utukufu Wako uje juu yangu, na ndipo nita—nitajua basi ya kwamba ilimaanisha—ilimaanisha hivyo, na kwa hiyo niweze kulinyamazia.” Wala hakuna jambo lililotukia.

³⁹ Kwa hiyo basi nikasema, “Basi, Bwana, kama lilimaanisha ya kwamba Wewe utawatuma Wajumbe Wako kwa ajili ya agizo langu, basi jalia nguvu Zako zije tena.” Karibu zinitoe humo chumbani!

⁴⁰ Hata hivyo, ni—nikajirudia, huku Biblia hii ikiwa mkononi mwangu, basi, mnaona, na nikimsihi Mungu anisaidie. Na nilipofanya hivyo, Yeye—Yeye alinionyesha jambo fulani katika Maandiko, linalohusiana nalo kabisa, papo hapo. Ndipo nikawazia, “Hilo kweli lingeweza kuwa ndilo hilo? Nilifanyaje jambo hilo?” Na, loo, si—siwezi kuyaelezea mambo haya, enyi watu. Ni zaidi ya chochote ninachojua habari zake. Mnaona?

⁴¹ Mke wangu ni mwanamke wa kipekee sana; mmoja wa walio bora sana ulimwenguni. Lakini, kitambo kidogo, sikusema lolote kulihusu. Niliendelea. Alijua jambo fulani lilikuwa limetukia. Kwa hiyo wakati nilipomwambia, yeye alisema, “Unajua, Bill, ninakuona na kukusikia, katika mengi ya mambo hayo.” Kasema, “Unajua ninakuamini kwa moyo wangu wote,” akasema. Akasema, “Lakini hilo kweli lilikuwa na kitu fulani.”

⁴² Linaonekana tu, linanitetemesha tu, huo mlipuko na mwendo huo wa kasi sana wa hao Malaika namna hiyo, watano wao pamoja, katika ku—kundi Lao. Kama, kwa namna fulani ni

kama—kama vile nilivyoichora ile piramidi hapa, mnaona, Wao walionekana namna hiyo. Kwanza, ilionekana kama, kwa namna fulani. . . wakiwa mbali, walionekana kidogo kama ile rangi ya hua. Nao walikuwa katika—wakiwa wanatokea upande *huu*. Nao, inaonekana kama: moja, mbili; tatu, nne; na halafu mmoja moja kwa moja juu, mnaona, ikifanya watano. Nao walikuja kasi mno! Hakuna kitu, hakuna jeti, hakuna kitu chochote kinachoweza kulinganishwa na *hao*.

⁴³ Nami ninaweza tu kuwaona, na vichwa Vyao kwa namna fulani vimegeuzwa upande mmoja. Hayo mabawa yameelekea nyuma, wamejihami vilivyo, nao hawa hapa wanakuja, kwa hiyo “Whiii!” Namna *hiyo*. Wakashuka tu moja kwa moja, nao wakanichukua moja kwa moja wakaniingiza ndani ya piramidi hii ya kundi Lao. Niliona ya kwamba nilikuwa nimeondolewa, nimeondolewa ardhini. Nikawazia labda. . . Nikasikia, huko mbali sana, huo mngurumo, “Vuum!” Kama nde—nde—ndege wakati inapovuka mapatano ya spidi ya ndege na sauti, mmeusikia ukitokea namna hiyo, kama tu mngurumo wa mbali.

⁴⁴ Nikawazia, “Hii inaweza kumaanisha sasa, wakati sasa ono hili litakaponiacha, ya kwamba nitauawa katika mlipuko ama kitu fulani.” Nikawazia, “Mimi hapa. Nimeinuliwa juu. Mimi ni. . . Wao, Wao wako hapa mahali fulani. Mimi ni—niko katika hii, piramidi hii ya Malaika hapa. Lakini, si—sijui. Labda Bwana anakuja kunichukua anipeleke Nyumbani.”

Ndipo nikamsikia Joseph huko chini, akisema, “Baba?”

Nikawazia, “La, kama ni hivyo, ungalimchukua, pia.”

⁴⁵ Ndipo Kitu fulani kikasema, “Wewe. . .” Kumbukeni, ninangojea, ninautarajia Ujumbe ambao daima nimeutazamia, jambo fulani.

⁴⁶ Nalo hilo ono, hivi majuzi, mwajua, kama nilivyolisimulia hapa si muda mrefu uliopita, likiniambia kile kilichokuwa kinaenda kutukia; jinsi nilivyokuwa nikihubiri katika, kutoka kwenye jua, kuelekea mahali hapa. Na—na halafu akasema, “Sasa kumbukeni, upeo wa pili wa mambo bado ungali unakuja.”

Nikawazia, “Kutakuwako na Ujumbe fulani.”

⁴⁷ Mnaukumbuka Ujumbe wangu hapa? Kule kufunguliwa kwa lile jiwe la kifuniko, ambapo, zile sauti saba na mihuri ambayo hata haijaandikwa katika Neno la Mungu. Mnaukumbuka? Nao wakaniingiza kwenye piramidi hiyo.

⁴⁸ Na Junie Jackson, kama upo hapa, ile ndoto uliyonipa si muda mrefu uliopita. Sitaisimulia asubuhi ya leo. Ulikuwa ninii sana. . . Mungu alikuwa kikamilifu sana. Na samahani kwa kutokukupata tafsiri yake; maana, niliona kitu fulani kikisogea.

J.T., jambo lile lile, mnaona. Na mimi—mimi—mimi nilijua hilo.

Na Dada Collins, jambo lile lile hasa. Unaona?

Na sita za hizo, zikielekeza moja kwa moja kwenye jambo lile lile.

⁴⁹ Halafu lile ono nililowaambia ninyi nyote, miaka kadhaa iliyopita, lilitukia tu hivi majuzi. Mnaona? Hilo lingetukia.

⁵⁰ Na hilo hapo, limewekwa sawa, kila kitu kimewekwa moja kwa moja hapo. Ni kitu fulani tu kinachosogea. Sijui ni kitu gani. Mungu anisaidie; ndilo ombi langu.

Na tuombe.

⁵¹ Baba wa Mbinguni, sisi—sisi ni wanadamu tu, na sisi hapa tumesimama asubuhi ya leo. Na, Bwana, umenituma kuliongoza kundi hili dogo na kanisa hili. Nami niko katika mwisho wangu. Sijui ni njia gani, ni nini, ni wapi, unanijia. Bali ninajua jambo hili moja, ya kwamba, Wewe ulisema ungefanya “kila kitu kitende kazi kwa manufaa” ya wale waliokupenda na wameitwa kulingana na kusudi Lako. Ninakuomba Wewe, Mungu, ya kwamba mkono Wako mkuu wa rehema utakuwa juu yetu.

⁵² Kweli tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu. Nasi tunajua ya kwamba Wewe siwe uliyeishi katika siku zilizopita, bali ungali unaishi leo hii. Daima Wewe ulikuwa ni Mungu. Daima utakuwa ni Mungu. Ulikuwa Mungu kabla ya wakati, Nawe utakuwa Mungu wakati hakutakuwako na wakati. Ungali utakuwa ni Mungu.

⁵³ Nasi tumo mikononi Mwako, Bwana. Sisi ni udongo tu, Nawe ni Mwenye Kufinyanga, Mfinyanzi. Yaumbe maisha yetu, Bwana, kwa njia ambayo tungepata utumishi ulio bora sana wa kukuheshimu. Tujalie, Baba. Tumo tu mikononi Mwako.

⁵⁴ Hatukuwa na njia ya kujileta wenyewe hapa, ama hatujui jinsi tutakavyoondoka. Bwana, Wewe ulitupa Uzima, Nawe umeninii. . . Tunayatoa maisha yetu Kwako tena, na, katika hilo, Wewe umetupa, badala yake, Uzima wa Milele. Imani yetu huleta jambo hilo katika utu wetu wenyewe. Nasi tunakupenda kwa ajili ya jambo hili, kwa maana tunajua ya kwamba siku moja tutakuona Wewe, Nawe utakuwa katika utukufu Wako. Nasi tutamwangalia Yeye. Nasi tunatamani kuyasikia maneno hayo, “Ni vema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu. Ingia katika furaha za Bwana, ulizoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Mpaka wakati huo, Ee Mungu, tutakapokutana sote, tuongoze.

Sisi ni watumishi Wako, na tunaomba msamaha wa dhambi zetu.

⁵⁵ Maono haya yenye nguvu, Bwana, yamezidi sana kwa mtumishi Wako. Sijui la kufanya. Mimi—mimi najua tu yanakuja. Nami ninaweza tu kusema yale niliyoona, na vile ilivyosemwa. Na wakati mwingine linaniogopesha sana, Bwana. Na si—sijui la kufanya.

56 Ndipo ninaichukua Biblia na kusoma humo ndani jinsi Isaya hapana budi alijisikia siku hiyo mle hekaluni, wakati alipowaona hao Malaika, mabawa juu ya miguu Yao. Si ajabu alilia, “Ole wangu, kwa kuwa macho yangu yameona utukufu wa Bwana.”

57 Na hapo ndipo nabii alipaza sauti: akiisha kusafishwa mle hekaluni, wakati yule Malaika alipochukua makoleo na kuchukua kaa la Moto na kuliweka juu ya midomo yake; baada ya kukiri ya kwamba alikuwa ni mtu mwenye midomo michafu, na akiishi na, miongoni mwa watu wachafu. Hata hivyo, yeye alikuwa ni nabii. Malaika alichukua makoleo na kuweka kaa la moto juu ya midomo yake na kumsafisha, na kusema, “Sasa nenda, ukatabiri.”

Bwana Mungu, Isaya alipiga kelele, “Mimi hapa, Bwana. Nitume mimi.”

58 Wakati, Yeye aliposema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?” Kwa ajili ya kizazi hicho kiovu na cha zinaa!

59 Ee Mungu, jalia lirudie tena. Jalia lirudi tena, Ee Bwana. Mtume Roho Mtakatifu akiwa na Moto usafishao. Kwa maana, ninakiri, mimi ni mwenye midomo michafu, na ninaishi katika dunia hii hapa pamoja na watu wachafu. Nasi ni wachafu machoni Pako, Bwana. Lakini, loo, tuma nguvu za utakaso, Roho Mtakatifu! Tusafishe, Ee Bwana. Msafishe mtumishi Wako, Bwana.

60 Kisha unene, Bwana. Mtumishi Wako anasikiliza. Nina shauku ya kusikia Sauti hiyo. Mimi ni Wako. Nitumie, Bwana, unavyoona yafaa, wakati nikijilaza juu ya madhabahu Yako. Jalia Roho Mtakatifu anisafishe, Bwana; na anitie mafuta na kunituma, Bwana, kama unataka mtu aende, kama hii ndiyo ile saa na huu ndio ule wakati.

61 Si—sijui, Bwana. Na—najua tu ya kwamba niliwaona wale Malaika. Nawe unajua mambo hayo kwamba ni Kweli kabisa. Nami ninaomba, Bwana, “Ole wangu,” kwa hiyo nisaidie.

62 Na sasa wabariki watu hawa. Nasi tupo hapa leo, kabla tu ya mkesha wa wakati huu wa sherehe za kuzaliwa kwa Bwana wetu. Tunaomba ya kwamba utatusaidia.

63 Na asubuhi ya leo, mtumishi Wako, Ndugu yetu Neville, amejisikia ya kwamba labda ingekuwa ni wakati ambapo anapaswa tu kupumzika muda kidogo, na labda mimi nihubiri. Nami na—naomba ya kwamba utanisaidia sasa.

64 Kuna wale hapa, Bwana, na sisi sote, tunakuhitaji Wewe. Kwa hiyo tunaomba sasa ya kwamba Wewe utatubariki tunapolisoma Neno Lako na kutafakari kwa kitambo kidogo. Jalia Roho Wako aje juu yetu, Bwana. Na utusafishe na kutuwasha Moto, na Roho Mtakatifu, kwa Ujumbe wa Mungu, mpya kutoka madhabahuni, kuutikisa ulimwengu unaokufa,

kabla ya kuja kwa yule Mungu mkuu wa Milele. Kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu, Mwanawe mpendwa, na Mwokozi wetu. Amina.

⁶⁵ Sasa ninataka kuelekeza usikivu wenu kwenye Maandiko fulani hapa, na mihtasari michache, ambayo nimeandika hapa.

⁶⁶ Na ninaamini, Doc, Billy, ama mmoja wao aliniambia, ya kwamba wanataka waachiliwe mapema kidogo, kwa ajili ya watoto wadogo. Wana zawadi kwa hilo.

⁶⁷ Ninyi jamaa wadogo ambao ndio kwanza mtoke kwenye shule yenu ya Jumapili, ka—kaeni tu humu, kwa muda mfupi tu. Yale tunayosema kutoka hapa huenda yakawa ni ya kina sana kwenu, bali ninyi—bali ninyi ketini tu kimya pamoja na mama na baba, kwa dakika chache. Ninataka kuzungumza nao.

⁶⁸ Sasa, katika Zaburi, Zaburi ya 89, ninataka kusoma kifungu kimoja ama viwili, vya Zaburi ya 89. Nitajaribu kusoma vifungu vya 50, 51, na 52 vya Zaburi 89.

⁶⁹ Sasa, mnaweza kusikia huko nyuma kabisa, vema? Kama mnaweza, inueni mikono yenu. Kwa hiyo mimi...Ni ipi ambayo...Je! maikrofoni hizi zote zinafanya kazi? [Mtu fulani anasema, “Sijui.”—Mh.] Je! *hii* ni bora zaidi, ama *hii*? Ati *hii*? *Hii*? [“Hizi mbili upande huu zinafanya kazi.”] Papa hapa, ati *hizi* mbili upande huu? [“*Hii, hii, na hii.*”] Vema.

⁷⁰ Sasa, sijui kama wataunasa huu kwenye kanda au la. Kwa namna fulani ni tukio tu lisilotarajiwa asubuhi ya leo.

⁷¹ Ila msisahau sasa, mje na marafiki wenu wote. Nami na—nawatakeni mwe na hakika, karibu, mjaribu kuhudhuria mkutano wa Jumapili ijayo.

⁷² Karibuni watalimaliza kanisa hili hapa, nadhani. Nami nita—nitarudi kwa ajili ya jambo hili, kuhubiri hiyo Mihuri Saba, kama yakiwa ni mapenzi ya Mungu, kutoka kwenye Maandiko hapa.

⁷³ Katika Kitabu cha Zaburi, mlango wa 89, kuanzia kifungu cha 50. Sikilizeni kwa makini kusomwa kwa Neno sasa.

Ee Bwana, ukumbuke, wanavyosimangwa watumishi wako; jinsi ninavyostahimili kifuari mwangu masimango ya watu wengi;

Ambayo adui zako wamenisimanga, Ee BWANA, naam, wamezisimanga hatua za masihi wako.

Na ahimidiwe BWANA milele na milele. Amina na amina.

⁷⁴ Ningetaka kuzungumza nanyi kwa dakika chache juu ya... Ninawataka mtie hayo alama, kwanza, na kuyasoma hayo tena na tena, vizuri sana. Labda yanahitaji kusomwa tena sasa hivi. Sikilizeni kwa makini sasa. Mnaona?

Ee Bwana, ukumbuke, wanavyosimangwa watumishi wako; jinsi ninavyostahimili kifuani mwangu masimango ya watu wengi;

Ambayo adui zako wamenisimanga, Ee BWANA, naam, wamezisimanga hatua za masihi wako.

Na ahimidiwe BWANA milele na milele. Amina na amina.

⁷⁵ Yasomeni kwa makini, kama yalivyonenwa na Daudi. Ninataka kutumia kama somo. . . Ni la ajabu sana, kama somo la Krismasi tena; lakini kama nilivyohubiri Jumapili iliyopita juu ya somo la ajabu. Ninasahau lilikuwa ni somo gani sasa. Lilikuwa ninii. . . [Ndugu fulani anasema, “*Ulimwengu Unaporomoka.*”—Mh.] Ati nini? [“*Ulimwengu Unaporomoka.*”] Kuporomoka: *Ulimwengu Unaporomoka.*

⁷⁶ Sasa ninataka kutumia kama somo, Jumapili hii: *Dhihaka Kwa Sababu Ya Neno.* Sasa hebu nilirudie tena, vizuri sana. Dhi- . . . *Dhihaka Kwa Sababu Ya Neno.*

⁷⁷ Mungu ana wakati, na sababu ya wakati huo, kutimiza kazi Zake zote. Mungu anajua kile hasa atakachofanya. Sisi hatujui. Ilitupasa tu kulipokea kadiri Yeye anavyotupa. Lakini, Yeye amejua, wala hakuna kitu kinachoharibika kwa yale Ye—Yeye amepanga kufanya. Yote yatatukia. Hakuna budi kuwa, wakati mwingine, na mambo magumu na ya kuparuza, ili kuleta tu kitu cha kweli, asili ya kweli ya jambo hilo.

⁷⁸ Mnajua, mvua huzaliwa kwenye anga zilizochafuka, zilizokaa ovyoovy, radi za hapa na pale na mbingu zenye ngurumo. Na kama hatukupata mvua, tusingeishi. Lakini mnaona kile kinachohitajika kuileta mvua? Ngurumo, radi, vimulimuli, hasira. Na kutoka humo inakuja mvua.

⁷⁹ Mbegu haina budi kufa, kuoza, kuharibika, kunuka, na kurudi kwenye mavumbi ya nchi, kusudi ilete uhai mpya.

⁸⁰ Inahitaji kutwangwa kwa dhahabu, kuigeuza tena na tena, nyuma na mbele, na kutwangwa mpaka taka zote zimeondolewa ndani yake. Sio kwa sababu inang’aa, maana taka za chuma, ambazo zinajulikana kama dhahabu ya mjinga, hung’aa kama dhahabu halisi. Lakini, unaweka yote mawili pamoja. Unayaweka upande mmoja, ni vigumu kuyatenganisha. Lakini ukiyaweka pamoja, unaweza kuyatenganisha. Naye mtwangaji sikuzote hana budi kuitwanga mpaka a—aone sura yake mwenyewe ikiakisiwa katika dhahabu.

⁸¹ Na Mungu huweka wakati na ana kusudi kwa ajili ya kila kitu afanyacho. Hakuna kitu kinachotukia kwa bahati mbaya tu kwa wale wampendao Bwana na wameitwa kulingana na wito Wake. Mnaona? Tumechaguliwa tangu zamani. Na kila kitu hufanya kazi vizuri tu, kwa ajili ya jambo hilo, kwa kuwa Yeye hawezi kusema uongo. Naye alisema hiyo ilikuwa ndivyo,

ya kwamba kila kitu kina wakati wake, majira yake, na kina njia yake. Na Mungu yuko nyuma ya kila msogeo. Na wakati mwingine unafikiri kwamba kila kitu kinaenda mrema. Ni juu yetu. Mambo hayo yanawekwa juu yetu, majaribu na fadhaa. Ni kujaribiwa, kuona vile tutakavyotenda kwa tukio fulani.

⁸² Wakati fulani uliopita katika, huko Vermont, mimi pamoja na Ndugu Fred tulienda huko upande wa New York, tukavuka Ziwa Champlain, nasi tulikuwa tumefika upande wa New York. Nami nikapanda juu ya mlima ambako, huko juu ya Mlima Hurricane, mahali nilipokuwa nikiwinda. Na hapo ninakumbuka wakati ambapo nilipotea, na jinsi ambavyo Mungu aliniongoza nikarudi, kwa Roho Mtakatifu tu, kupitia kwenye tufani. Kwamba, ningalikufa, niangamie, na vivyo hivyo mke wangu pamoja na Billy, huko chini kwenye kambi ndogo umbali wa maili kadhaa. Nami niligeuzwa nikarudi.

⁸³ Na kulikuwako na theluji kidogo tu tulimopitia, kuingia kambini, mapema kwenye msimu wa kuchipua. Nami nilikuwa nimesimama pale nikizungumza na Ndugu Fred, basi Roho Mtakatifu akasema, “Nenda uwe peke yako.” Ndipo nikaingia kichakani kwa muda kidogo, mahali. Akaniambia, “Kuna mtego uliotegewa. Kuwa mwangalifu sasa.” Bali hakuniambia ni vipi, ni nini. Nikarudi nikamwambia Ndugu Fred.

⁸⁴ Tukaenda kanisani usiku huo katika jumba la mikutano, nikalitangaza kwa watu. Na kesho yake usiku likatendeka. Halafu akisimama pale wakati aliponiambia, kuhusu wenye dhihaka fulani, Yeye alisema, “Liko mikononi mwako. Fanya utakalo nao. Lolote usemalo, litatukia sasa hivi.”

⁸⁵ Haya basi. Ambapo, mtu asiye na kicho, asiye mcha Mungu, nao walikuwa wakidhihaki na kufanya mzaha mkutanoni, kijana mwanamume na kijana mwanamke. Naye alikuwa akijaribu kufanya mapenzi machafu pamoja naye jengoni, na kuuvutia usikivu wa kila mtu, wakati nilipokuwa nikichachamaa kuhubiri. Basi anavuta kichwa chake nyuma na kupanda juu ya paja lake, na kusukuma kichwa chake nyuma na kujaribu kumbusu, na kuendelea namna hiyo kwenye mkutano, akiuvutia usikivu.

⁸⁶ Ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Sasa huyo ni... Wako mikononi mwako. Utafanyaje nao?”

⁸⁷ Kulikuwako na ukimya mtakatifu. Kila mtu aliketi kimya cha mauti. Nami nikawaza, “Ee Mungu, nifanyeje?”

⁸⁸ Ndipo nikakumbuka, kama isingalikuwa ni lile onyo la Roho Mtakatifu, siku mbili hapo kabla. Nikasema, “Nitawasamehe.” Sasa, hilo ndilo Yeye alinitaka niseme. Mnaona?

⁸⁹ Kwa sababu, hata hivyo, ni—nimekuwa na hatia, labda si ya aina hiyo, bali hatia. “Na aliye na hatia kwa neno lililo dogo sana amekosa juu ya yote.”

⁹⁰ Kwa hiyo nikasema, “Ninawasamehe.” Na kuna mashahidi wanaoketi hapa sasa, waliokuwa pale wakati huo. Halafu Roho Mtakatifu akashuka.

⁹¹ Sasa, mnaona, ninaamini ya kwamba mambo haya yote yalikuwa na maana. Ungefanya nini na nguvu? Ungefanyaje, unaona, tendo la kujibu tukio? Kitu ambacho kimetokea kama tukio, basi unafanyaje kwa tukio hilo? Mnaelewa ninalomaanisha? Ungefanya nini? Na labda mambo haya yote yametukia kutufikisha mahali tulipo sasa. Sijui. Si—siwezi kusema kamwe. Lakini sikuzote kumekuwako na njia fulani.

⁹² Basi kumbukeni kwamba, dhihaka juu ya—juu ya Neno imekuwa. . . Neno sikuzote limestahimili dhihaka. Kote katika nyakati, Neno la Mungu lililotiwa mafuta daima limedhihakiwa. Na hiyo ndiyo sababu ni vigumu sana kwa watu ambao hawaelewi, wangejua jinsi ya kuikubali dhihaka hiyo.

⁹³ Je! mnaweza kukumbuka wale wanafunzi wakirudi na kufurahi kwa sababu walijiona kwamba walihesabiwa kuwa wanastahili kustahimili dhihaka ya Jina Lake? Yeye alisema, “Wote wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo wataudhiwa,” dhihaka ya Neno.

⁹⁴ Huna budi kustahimili dhihaka hii kusudi upate majaribu yako, kuona. Kila mtu amjiaye Kristo hana budi kufundishwa kama mtoto kwanza, kwa ku—kusudi ambalo Mungu amekuchagulia. Pia kumbuka, laiti ungeweza kunyamaza tu! Kumbuka, kama Yeye amekuitia jambo hili, hakuna kitu kinachoweza kulizuia kutukia. Hakuna pepo wa kutosha matesoni, ila kwamba Neno la Mungu litadhihirishwa. Umezaliwa kwa kusudi fulani, wala hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Huenda ukawa na waigaji na chochote kile, bali kamwe hawatapachukua mahali pako. Vema. Neno la Mungu litashinda. Haliwezi kushindwa. Hapo ndipo ambapo kila Mkristo anapaswa kusimama, akijua jambo hilo—hilo. Nayo majaribu yataibuka, na yaonekane kwa kila njia, kwako. Bali kumbuka, Mungu ana kusudi, na yote yatakuwa sawa.

⁹⁵ Sasa hebu turejee nyuma kwenye matukio ma—machache ya kutimizwa kwa Neno la Mungu, na wale waliolichukua Neno katika wakati wao.

⁹⁶ Ni—nilijisikia katika Roho, si muda mrefu uliopita, ya kwamba mtu fulani alikuwa akinikosoa. Huenda ilikuwa ni katika ulimwengu wa kanda. Juu ya daima kurejea sana, kurejea nyuma na kuchukua watu wa Biblia kuhusu yale ninayosema. Vema, ninafanya hivyo kwa kusudi fulani. Biblia ilisema mambo haya yameandikwa kusudi tuyaangalie. Na hiyo ndiyo njia pekee, bila ya elimu, jinsi tu ninavyoweza kufanya, ni kurejea nyuma na kusema, “Mnaona mahali *hili* linaposimama, kile

kilichotukia kwake, ambapo *hili* lilitukia.” Mnaona? Na ndipo unajiweka tu mwenyewe pale.

⁹⁷ Kama vile nilivyokuwa nikihubiri, si muda mrefu uliopita, juu ya maskini mvulana mdogo huko nje kwenye meli, mwajua, na—na maskini mzee nahodha alikuwa akifa. Alikuwa ni mgonjwa. Ndipo akauliza kama hakukuwako na Biblia melini. Nao wakampata mvulana mdogo aliyekuwa na Biblia, naye akaja na kusoma Isaya 53:5. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa uovu wetu.” Ndipo akasema, “Hebu... Hebu nikwambie, nahodha, jinsi mama yangu alivyokuwa akipasoma.” Kasema, “Hivi ndivyo alivyoliandika. ‘Alijeruhiwa kwa ajili ya uovu wa Willy Pruitt. Na aliadhibiwa kwa ajili ya Willy Pruitt. Na mambo haya yote aliyofanyiwa, yalikuwa ni kwa ajili ya Willy Pruitt.’” Hilo lilikuwa ndilo jina lake.

Maskini nahodha akasema, “Ninapenda jambo hilo. Je! waweza kusoma jina langu ndani yake?”

⁹⁸ Akasema, “Nitajaribu.” Naye akasema, “Alijeruhiwa kwa makosa ya John Quartz. Alichubuliwa kwa uovu wa John Quartz. Na kwa mapigo yake John Quartz aliponywa.”

Akasema, “Ninaliona.” Na Bwana akamponya. Unaona?

⁹⁹ Soma jina lako ndani yake. Alijeruhiwa kwa ajili ya makosa ya William Branham. Alichubuliwa kwa ajili ya uovu wa William Branham. Alifanya hivyo kwa ajili yangu, na alifanya hivyo kwa ajili yako. Soma jina lako katika hilo.

¹⁰⁰ Vema, hivyo ndivyo ninavyopenda kuyaleta Maandiko kwa watu wa—wangu, ni yale aliyomfanyia mtu mwingine ambaye alimtii. Yale aliyomfanyia mtu mwingine ambaye alikuwa mwaminifu kwa Huduma, na yale aliyomfanyia mtu mwingine ambaye hakuwa mwaminifu kwa Huduma, basi wewe unasoma jina lako ndani yake. Kama wewe ungalikuwako pale, ungalichukua msimamo gani? Pia kumbuka, una majaliwa, siku hizi, kuchukua msimamo wa namna iyo hiyo.

¹⁰¹ Wakati, Nuhu, juu ya dhihaka ya Neno ambalo Mungu alinena naye. Nuhu, kulikuwako na dhihaka. Nuhu aliishi katika wakati wa sayansi, ambapo kulikuwako na mafanikio ya sayansi waliyoweza kuunda, ambayo yalikuwa ni ya juu sana kuliko chochote ambacho tumepata kuunda siku hizi. Walikuwa werevu zaidi, wenye akili zaidi. Sayansi yao ilikuwa imeenda mbele sana, kuliko yetu. Pia kumbukeni tu, ilimbidi kuistahimili dhihaka ya Neno ambalo alihubiri, miaka mia moja na ishirini, mbele ya wenye kudhihaki. Njia zao kuu za sayansi ziliwathibitishia ya kwamba hakukuwako na mvua angani. Lakini, hata hivyo, Nuhu alikuwa amelisikia Neno la Bwana, nalo lilikuwa ni kinyume na dhana zao za jambo Hilo. Kwa hiyo, kabla uhai wake haujaweza kuokolewa, hana budi kusimama kukabiliana na kubeba dhihaka ambayo hawa wenye kudhihaki walimdhihaki nayo.

¹⁰² Loo, hapana shaka, hapana budi walimwonea huruma maskini mhubiri huyo mzee. Hawakumfukuza ama chochote kile, kwa sababu labda hakukuwako na nyumba nyingi za aina hiyo katika siku hiyo. Hakuwa na madhara. Asingemdhuru mtu yeyote, kwa hiyo waliachana tu naye. “Endelea, maskini mzee mlokole huko juu kwenye mimba ya kilima, akijenga meli huko nje mbali ambako hakuna maji. Loo, vema, maskini jamaa huyo mzee! Lakini,” na kusema, “utayapata wapi maji yako, ya kufanya mashua yako iele, Nuhu?”

“Itanyesha kutoka mbinguni.”

¹⁰³ “Upuuzi. Tunaweza kurusha chombo kwenye jua na nyota, kwa rada,” chochote walichokuwa nacho. “Hakuna mvua huko juu.”

Lakini akasema, “Mungu alisema Yeye ataweka mvua huko juu.”

“Atafanyaje jambo hilo?”

¹⁰⁴ “Hiyo ni kazi Yake. Jambo pekee ninalopaswa kufanya ni kuwaonya mtoke hapa.”

¹⁰⁵ Ni karibu tu kama ilivyo sasa. “Huo moto unatoka wapi?” Ndugu, ni dhahiri kidogo zaidi siku hizi kuliko ilivyokuwa wakati wa Nuhu. Tayari tunauona mahali ulipo. Uko tayari tu kupiga, hivyo tu. Sayansi tayari imeninii. . . Hakuna udhuru wakati huu, hata kidogo, maana sayansi tayari imeupata. Naam, bwana.

¹⁰⁶ Kwa hiyo sasa tunaona ya kwamba lilikuwa ni jambo zito. Kwa hiyo walimwonea huruma maskini mhubiri huyo mzee, na kumwacha tu aendele. Lilikuwa ni jambo la kigeni, labda, kwa hao watu, kuwazia ya kwamba mtu aliyeaminiwa kuwa ana akili, na angeamini ya kwamba Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, angefanya jambo fulani, ama kusema jambo fulani ambalo alikuwa atafanya, ambalo lilikuwa ni kinyume na mawazo yao, yale waliyokuwa nayo. Labda hamkulipata. Angalieni. Ilikuwa. . . Walidhani ya kwamba wangeweza kuthibitisha kila kitu cha maumbile ya kawaida kwa sayansi yao. Kama huo haufanani na ulimwengu tunamoishi siku hizi, ulimwengu wenye akili, wenye elimu, uliojaa sayansi! Na chochote ambacho wangiweza kuthibitisha, kilichokuwa ni makosa, ninii ya Mungu. . . “Hakuna Mungu angaliweza kamwe kunena chochote ambacho (kilichokuwa) kingeweza kuthibitishwa kisayansi kwamba hakikuwako.”

¹⁰⁷ Sasa, wana wazo lile lile siku hizi. Kama daktari wako akisema ya kwamba una kansa, huna budi kufa, nayo sayansi inathibitisha ya kwamba una kansa, nayo imeenea sana, ni ujinga kuwazia vinginevyo, kwa sababu utakufa; hivyo tu. Sayansi inasema utakufa. Wamekuchunguza, na hakuna lingine la zaidi. Utakufa. Nao wanafikiri ni wendawazimu kama ukijaribu kusema ya kwamba Mungu aliahidi kufanya jambo

hilo. Mnaona, kama vile ilivyokuwa, huna budi kustahimili dhihaka hiyo.

¹⁰⁸ Wao wanasema, kama daktari anasema hapa, “Tulichunguza kila kitu, na hiyo kansa imeenea. Tulikufanyia upasuaji. Imejaa kote mwilini mwako, na kote moyoni mwako, kwenye mapafu yako yote, kwenye ini lako lote, kila mahali. Haiwezekani.”

Kwa hiyo, unaona, unaposema, “Lakini ataishi, hata hivyo.”

Wao wanasema, “Vema, maskini jamaa huyo, achana tu naye.”

¹⁰⁹ Ninakumbuka usiku ule. Bill Hall, Ndugu Hall huko kwenye kanisa la Milltown, wengi wenu mnakumbuka kisa hicho. Na wakati yeye... Walinipigia simu. Mimi, mke wangu na mama mkwe, tukatoka tukaenda hapa. Alioa msichana aliyekuwa ni dada, ninaamini, wa George Cupp, aliyekuwa meya wa mji, ama hakimu hapa. Nanii wake... Huyo alikuwa ni shemeji yake wa kiume. Walimleta hapa kuja kufa. Daktari wa huko Milltown, daktari wa New Albany, waliubaini ugonjwa huo kama kansa ya ini. Kwa hiyo nikashuka kwenda kumwona Bibi Hall. Naye alikuwa ameshikwa na homa ya nyongo ya manjano, naye alikuwa manjano mwili mzima. Ndipo nikasema, “Vema, nadhani atakufa.” Nami nikasema...

¹¹⁰ Akasema, “Ndugu Bill, je! kuna njia yoyote ambayo imeninii... Je! unaweza kusikia kutoka kwa Mungu?”

Nikasema, “Mimi—mimi sijui, Dada Hall. Ninaweza kuomba.”

¹¹¹ Nikaomba. Kisha nikarudi nyumbani, wala Bwana hakuniambia kitu. Kisha nikarudi, kesho yake, na nikaomba tena.

Naye akasema, “Je! unamjua daktari yeyote mzuri?”

¹¹² Nikasema, “Vema daktari wa familia yetu ni Dk. Sam Adair, hapa chini Jeffersonville. Yeye ni—yeye ni—yeye ni... Baba yake alikuwa daktari wa familia yetu. Mimi na Sam mdogo daima tumekuwa marafiki wasiri, na—na tulienda shuleni karibu wakati mmoja, tulilelewa pamoja. Sikuzote tunamwendea pindi jambo lolote baya likitokea.”

Akasema, “Sijui kama angekuja kumwalia Bill Hall?” mumewe.

Nikasema, “Nitamwalika.”

¹¹³ Vema, Sam akaniambia, akasema, “Billy, kama daktari alisema ana kansa,” kasema, “kuna jambo moja tu, la mimi kufanya, nitampeleka kwa mtu aliye mwerevu kuliko mimi, kwa mtaalamu. Nasi tutachukua ekisi-rei; wala hatutamwingiza kwenye shida yoyote tena.”

¹¹⁴ Tukaenda New Albany na kuchukua ekisi-rei kutoka kwa daktari huko chini. Tukampeleka Louisville na kumchunguza, tukampeleka huko na ambalanzi, kisha tukamrudisha.

¹¹⁵ Vema, kweli, asingemwambia Bibi Hall kwamba shida yake ilikuwa ni nini, kwa hiyo akanipigia simu. Akasema, “Atakufa,” kasema, “rafiki yako mhubiri.” Kasema, “Yule daktari bingwa huko Louisville amenipigia simu sasa hivi, na kusema, ‘Ule ubaini uliotolewa na madaktari katika—katika... huko Milltown; na daktari, New Albany; ulitoa ubaini wa kweli.’” Kisha kasema, “Ni kansa ya ini, nayo imeenea. Na, Billy, hatuwezi kulikata ini la mtu huyo, na aishi.” Kasema, “Atakufa. Na kama yeye ni mhubiri, anapaswa kuwa tayari.”

¹¹⁶ Nikasema, “Hilo silo swali. Lakini yeye hajakipita umri wa miaka hamsini na mitano, kwa hiyo angali ana uhai mwingi ndani yake bado, wa kuhubiri.” Kisha nikasema, “Vema, kama atakufa, hilo linamaliza mambo basi. Asante, Dk. Sam.”

¹¹⁷ Basi nikashuka nikaenda nikampigia simu Bibi Hall, na nikamwambia. Nikasema, “Bibi Hall, Sam amesema ubaini wa Louisville kule ulikuwa ni kama wa New Albany na Milltown. Mtu huyo anakufa. Ndugu Hall atakufa. Naye ana kansa kwenye ini, na imeenea.”

¹¹⁸ Na kwa hiyo akaanza kulia. Nikageuka, nikaomba pamoja na mumewe. Naye alikuwa hajitambui kabisa, wakati huo, hata hakujua nilikuwa humo chumbani.

¹¹⁹ Kwa hiyo, nikarudi. Na watu wengi walikuwa wamekuja hapo nyumbani, siku hizo. Hakukuwa na mtu mwingine hudumani. Haikuwa imetiwa uchafu na mambo mengi sana, nao watu walikuwa wakija kutoka kila mahali.

¹²⁰ Nilitaka kupumzika kidogo. Kwa hiyo nikaingia kisiri, nikaamka mapema, yapata saa nane na nusu, ama saa tisa. Ndugu Wood hakuwa amehamia uchorochoroni bado. Basi nikaangalia huko barabarani, wala hakukuwako, hakuna mtu huko nje, kwa hiyo nikachukua kofia yangu chakavu nikaingia upesi kwenye chumba cha faragha, nikachukua bunduki yangu ya.22. Nami nilikuwa nikitaka kutoka nikawinde kuchakulo, mpaka ifikie kama saa mbili, kisha nilale karibu na mti mahali fulani na nijipatie usingizi mdogo. Usingeweza kuupata nyumbani.

¹²¹ Nikaichukua kofia yangu nikaanza kutoka humo chumbani. Tofaa lilikuwa likining’inia ukutani. Nalo lilikuwa ni tofaa lililonajisiwa zaidi. Lilikuwa limeliwa na minyoo, nalo limejaa vifundo, na limejaa uchafu kila mahali. Ndipo nikawazia, “Ni kwa nini Meda alitundika hilo ukutani?”

¹²² Ndipo nikaangalia, tena, na halikuwa ukutani. Lilikuwa limening’inia hewani. Nikavua kofia yangu kuukuu mara moja, nikaiweka bunduki pembeni, nikapiga magoti. Nikasema, “Bwana, ungetaka mtumishi Wako ajue nini?”

¹²³ Likashuka lingine, moja kwa moja likashuka lingine, mpaka karibu matofaa manne ama matano (ninasahau sasa yalikuwa ni mangapi) yalining'inia pale. Ndipo tofaa kubwa mno, la kupendeza, lenye milia ndani yake; tofaa kubwa mno, linaloonekana kuwa na afya, likashuka na kuyala kwa pupa hayo matofaa mengine yaliyoonekana magonjwa. Naye akasema, “Amka. Simama kwa miguu yako.” Kasema, “Nenda kamwambie Bill Hall, yeye hatakufa. Ataishi.”

¹²⁴ Loo, nikakimbia upesi nilivyoweza, na nikasema, “Bibi Hall, nina BWANA ASEMA HIVI. Yeye ataishi.” Naye mume akanisikia. Naye alikuwa akijaribu kulia, wala asingeweza kuzungumza tena.

¹²⁵ Nikarudi na kumpigia Sam simu. Nami nikasema, “Sam, ndugu ye—yetu ataishi.”

Akasema, “Anawezaje kuishi namna hiyo?”

¹²⁶ Nikasema, “Hilo si juu yangu kuliwazia. Mungu alisema hivyo. Hilo latosha.”

¹²⁷ Yeye yu hai leo hii. Hiyo imekuwa ni karibu miaka kumi iliyopita. Mwenye nguvu tu na afya. Mkewe amekufa tangu wakati huo. Ameoa tena.

¹²⁸ Itakuwaje kwa George Wright, na wengi zaidi tunaoweza kusema, tunaoweza kuwataja? Ni kitu gani? Ni kuistahimili dhihaka. Wanacheka na kudhihaki.

¹²⁹ Ninakumbuka hapo kabla ya mafuriko ya mwaka wa '37, nilisimama pale na Kampuni ya Uhamishaji ya Jiji la Falls, nami nilikuwa nikiwaambia kuhusu, kutakuwako na futi thelathini na mbili za maji, ninaamini ilikuwa hivyo, kwenye Barabara ya Spring. Walinicheka. Wakasema, “Maskini Billy. Nadhani yeye. . . Maskini mtoto huyo!” Nilikuwa mvulana tu wakati huo. Akasema, “Billy ni mtoto mzuri. Ni aibu yeye amechanganyikiwa kabisa.” Sikuwa nimechanganyikiwa. Nilikuwa nimebatizwa *ndani*, sio kuchanganyikiwa. Nilikuwa tu niko “ndani.” Na lilitukia vivyo hivyo tu.

¹³⁰ Tangu nimekuwa nikihubiri, nilimwona Dada Hattie Wright, ninaamini, ameketi pale nyuma. Anakumbuka kile kisa cha Bill Hall. Wengi! Ni wangapi hapa, waliopo asubuhi ya leo, wanakumbuka kisa hicho? Loo, jamani! Hakika. Kuna wengi wenu.

¹³¹ Sasa, wanatuhurumia, wanamhurumia mtu yeyote anayejaribu kulishikilia Neno, katika siku za wenye kudhihaki. Lakini, kumbukeni, dhihaka haina budi kuja. Sikuzote imekuwa hivyo. Hapana shaka waliwazia, kama walivyofanya wakati huo, ya kwamba Mungu, baada ya kitu chochote kuthibitishwa kisayansi, ya kwamba Mungu asingeweza kunena chochote kilichokuwa kinyume na sayansi. Vema, hilo ndilo linalomfanya Yeye Mungu. Kama angalienda tu kulingana na sayansi,

basi isingekuwa ni zaidi ya vile tu mwanadamu angaliweza kufanikisha. Lakini, Yeye ni Mungu. Yeye Ndiye—Yeye Ndiye muumba wa sayansi. Anaweza kufanya kile anachotaka.

¹³² Hapana shaka waliwazia, “Maskini mzee Nuhu, vema, achaneni na mzee huyo. Yeye anakosa burudani zote tulizo nazo siku hizi, kwa hiyo achaneni tu naye.” Ni kama ni vivyo hivyo sasa.

¹³³ Lakini, sasa, ninataka kusema jambo lingine papa hapa. Sasa, tunaangalia nyuma na kuipenda imani yake. Lakini nashangaa, kama tungeishi katika siku ile, tungalichukua msimamo uo huo Nuhu aliouchukua? Je! tungeweza na tungekuwa tayari kustahimili dhihaka iliyoambatana na Kweli hiyo? Wakati, kati ya mamiloni yote yaliyokuwa ulimwenguni wakati huo, kulikuwako tu na Nuhu na familia yake walioitetea Kweli hiyo. Mliwazia jambo hilo? Ni mtu huyo tu na wanawe watatu, na wakaza wanawe, mke wake, ndio tu walioitetea hiyo Kweli. Lakini walikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Tunaangalia nyuma na kumpenda. Tunaweza kuliwazia tena?

Sina budi kuharakisha kwa sababu ya zawadi za watoto hawa.

¹³⁴ Ibrahimu, neno lenyewe *Ibrahimu* linamaanisha “baba wa mengi,” kumfanya “baba wa mataifa.”

¹³⁵ Sasa, Ibrahimu alilisikia Neno la Mungu. Ibrahimu alikuwa ni nabii, naye alilisikia Neno la Mungu. Nasi tunampenda Ibrahimu kwa ajili ya kushikilia kwake Neno la Mungu; jinsi ambavyo alijitenga na jamaa zake; jinsi ilivyokuwa ni vigumu kwa Ibrahimu. Yeye alilelewa kule juu. Alishuka kutoka Babeli, na—na alikuwa huko chini katika nchi ya Shinari na ya—ya—ya Wakaldayo, katika jiji la Uru, ambako wenzi wake wote, watu wake, na wote wale aliohudhuria kanisani nao, na kila kitu. Lakini Mungu alisema, “Jitenge.” Loo, jamani! Lilikuwa ni jambo la kutisha jinsi gani, kuacha yote yale aliyothamini, kila kitu kilichokuwa ni halisi kwake, alichokithamini. Na Mungu akamwambia, “Jitenge.”

¹³⁶ Na akampa kitu cha kipekee sana. “Utampata mtoto kwa mke wako.” Naye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na mke alikuwa na sitini na mitano. Alikoma katika desturi ya wanawake, katika desturi ya wanawake ya kuwaleta watoto, kwa miaka mingi. Na hapa, baada ya kuishi naye tangu alipokuwa msichana, kwa kuwa alikuwa ni dada yake wa kambo, halafu angaliwezaje kamwe kumzaa mtoto huyo? Na sasa ungeweza kumwazia Ibrahimu akitoka kwenda miongoni mwa marafiki zake, na kusema, “Tutapata mtoto, mimi na Sara”? Ungeweza kuwazia hilo?

¹³⁷ Mbona, watu hao walisema, “Maskini mzee huyo, ana kasoro fulani.”

138 Ni dhihaka, bali Ibrahimu aliishikilia. Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, kamwe hakusita kwa ahadi ya Mungu. Angali aliistahimili dhihaka, hakika, akiishikilia.

139 Mnaona tofauti katika jambo hilo? Sara alijaribu kumpa Ibrahimu, ama kumpa Mungu, hasa, msaada kidogo, kwa yeye mwenyewe. Aliwazia, mwajua, ya kwamba, vinginevyo zaidi ya vile Mungu alivyoahidi. “Sasa, mwajua, mimi ni mwanamke mkongwe, bali Hajiri hapa ni mwanamke mrembo. Ibrahimu hatajali kumwoa, pia. Kwa hiyo, mwajua, hilo—hilo litamsaidia Mungu. Hilo litamsaidia Mungu, maana Hajiri, hapa, labda ana umri wa miaka ishirini tu. Yeye ni mjakazi wangu. Na unajua nitakalofanya? Nitampa mume wangu, awe mkewe,” maana kuoa wake naye kulikuwa ni halali. Kwa hiyo akasema... “Nitampa yeye, naye atampata mtoto kwa mume wangu, halafu nitamchukua mtoto huyo. Na huyo ndiye, aliyeahidiwa na Mungu.”

140 Mnaona, sikuzote sisi hujaribu kufanya jambo fulani; hatuwezi kumngojea. Hatuna budi kufanya jambo fulani, sisi wenyewe. Huenda ilikuwa ni sawa. Huenda alikuwa ni mrembo. Huenda lionekane kuwa ni zuri sana, bali haikuwa ni kulingana na Neno. Mungu alimwambia Ibrahimu, “Mtoto huyo atakuja kwa Sara.”

141 Mnakumbuka kile alichosema kuhusu Kundi dogo? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, ambapo wachache, hasa watu wanane, waliokolewa.” Maneno hayo hayawezi kushindwa, kwa hilo hebu na tujiangalie wenyewe kwa makini na kudumu na hilo Neno. Vema. Unaona?

142 Watu daima wanajaribu kujibunia kitu fulani, kupachukua mahali pa mapenzi ya Mungu yaumbayo. Unaona, kama ambavyo nimesema daima, na labda mbele ya kanisa, hapo nyuma, unajua, usingeweza kumsihi kondoo, “Utanitengenezea sufu kidogo?” La, hawezi kufanya hivyo. Sasa, mbuzi hawezi kutengeneza sufu, kwa sababu asili yake isingemruhusu. Haidhuru ungejaribu kiasi gani kuifunga sufu ya kondoo juu ya mbuzi, haitafaa kitu. Mbuzi hawezi kutengeneza sufu, wala kondoo hatengenezi nywele. Lakini yeye ana sufu kwa sababu yeye ni kondoo. Hiyo ndiyo inayomfanya hivyo. Yeye hatengenezi.

143 Hutupaswi kutengeneza matunda ya Roho. Tunapaswa kuzaa tunda la Roho. Mtofaa hautengenezi matofaa; unayazaa tu kwa sababu ni mtofaa.

144 Na kama tukijaribu kutengeneza kitu chochote, “Nitaisaidia Huduma. Nitajifunza kwa muda wa miaka kumi katika seminari. Nitajifunza *hili, lile*, ama *linginelo*, na kupata Digrii

yangu ya Sanaa na ya Udaktari. Nitamsaidia Bwana, peke yangu.” Halitafaa kitu.

¹⁴⁵ Mungu, kwa kujua tangu zamani, humwita yule atakaye. Yeye humpa Ufalme yule Yeye atakaye kumpa. Tulijifunza hilo kwa Nebkadreza.

¹⁴⁶ Tulijifunza hilo kwa—kwa Yeremia. Wakati Mungu alipomwambia ya kwamba kwa Neno la Bwana, ya kwamba wakati unakuja ambapo Israeli watahamishwa wapelekwe Babeli kwa muda wa miaka sabini. Huyu hapa akaja nabii mwingine. Tayari alikuwa amemwambia, kasema, “Sasa, mtakuwa na manabii, watakaoinuka. Nanyi mtakuwa nao huko Babeli, watakaoinuka, na waota ndoto na manabii, ambao watatabiri kinyume na Hili. Lakini waambie watu wasiwasikilize watu hao.”

¹⁴⁷ Basi akainuka mtu jina la—lake, mmoja wa manabii, Hanania. Na wakati Yeremia alipokuwa amesimama pale amefungwa nira shingoni mwake, Hanania akaja, akasema, “BWANA ASEMA HIVI; katika miaka miwili kamili, vyombo vyote vya Bwana . . .” Sasa, kimsingi, lilionekana ni jambo zuri sana. “Mungu atawabariki watu Wake. Atarejesha kila kitu vivyo hivyo hasa, katika muda wa miaka miwili.”

¹⁴⁸ Nayo Biblia ilisema, hata nabii Yeremia alisema, “Amina. Amina. Hanania, Bwana na ayatimize maneno yako. Lakini hebu na tuwazie jambo fulani, Hanania. Kumekuwako na manabii kabla ya sisi, nao walitabiri dhidi ya mataifa makubwa ya vita, na kadhalika. Lakini, kumbuka, nabii hujulikana baada ya unabii wake kudhihirishwa.” Unaona?

¹⁴⁹ Ndipo Hanania akaja, akainyakua nira kutoka kwenye shingo ya Yeremia, mbele ya makuhani wote na kusanyiko, labda watu milioni moja na nusu. Na akaichukua nira hiyo ambayo Mungu alikuwa ameiweka juu ya shingo ya Yeremia, kama ishara, akaivunja vipande-vipande, na kuitupa miguuni pake, akiwa tu na mhemko, kisha akasema, “BWANA ASEMA HIVI; Katika miaka miwili, watarudi.”

¹⁵⁰ Yeremia alimwangalia tu. Ilikuwa ni kinyume cha Neno, kwa hiyo akajiondokea tu. Na Mungu akasema, “Rudi ukamwambie,” kasema, “Kamwe sikusema naye.”

¹⁵¹ Alikuwa tu amehemkwa. Alichukua tu wazo lake mwenyewe. Mnaona? Hakungojea mpaka kweli akaliona na kujua haikuwa ni yeye, ya kwamba ilikuwa ni Mungu anayelisema. Akarudi, amejaa mhemko. Kama . . .

¹⁵² Tunaliona, kote nchini, leo. Moja ya kanda zetu ilikuwa ikichezwa hivi majuzi katika nyumba moja, ambamo kundi la wahudumu walikuwa papo hapo wameshawishika, nao walikuwa wakija kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Ndipo mtu mmoja akasimama humo chumbani, aliyenena kwa lugha

na kusema, “BWANA ASEMA HIVI. Shikilieni yale mliyo nayo. Endeleeni tu, endeleeni, nami nitawabariki.”

¹⁵³ Wakasema, “Vema, kama Bwana alisema jambo hilo, nadhani hakuna lingine.” Unaona, halichunguzwi na Neno. Hapana budi kulichukua Neno, kwanza. Haya basi. Lilikuwa ni kinyume cha Neno.

¹⁵⁴ Huyu hapa Yeremia anarudi, huyo nabii aliyetiwa mafuta. Mungu alimwambia, kasema, “Ninajua Hanania aliivunja ile nira ya mbao kwenye shingo yako, niliyoiweka, bali nitafanya moja ya chuma.” Akasema, “Na mataifa haya yote ambayo yameshuka kwenda kumtumikia Nebkadreza, mtumishi Wangu,” naye alikuwa ni kafiri. Mnaona? Nao Israeli, wakishika dhabihu zao zote, bali hawakuwa . . . Mnaona?

¹⁵⁵ Mungu alifanya ahadi, ya kwamba angebariki, bali baraka hizo zina masharti. Nawe huna budi kutimiza masharti hayo, kuyafanya yatende kazi.

¹⁵⁶ Nikiketi, muda mfupi uliopita, pamoja na maskini msichana mdogo, mzuri sana hapa. Kwanza, niliihoji familia hiyo kila jambo, kuona kama kulikuwa na kasoro yoyote. Mungu ataponya, bali ni chini ya masharti. Mnaona? Jambo pekee tu nililopata, lilikuwa, mama alihofu ilikuwa ni makosa kunywa dawa. Nikasema, “Kamwe usiwazie hilo, dada. Ondoa jambo hilo ndani ya moyo wako. Endelea moja kwa moja na mtoto huyo. Mpe hiyo dawa. Mungu atafanya jambo hilo lijulikane.” Unaona?

¹⁵⁷ Sasa, lakini, hilo jambo ni kwamba, tafuta, ujue. Halafu, kama ni BWANA ASEMA HIVI, sawa.

¹⁵⁸ Sasa tunaona hapa ya kwamba, watu hawa, walikuwa wakijaribu kutengeneza kitu fulani; Hajiri na—na Sara, kumsaidia Ibrahimu, kumsaidia Mungu kuitimiza ahadi Yake. Huwezi kufanya jambo hilo. Hakuna njia, hata kidogo, ya kufanya jambo hilo. Ni—ni kinyume na kila kitu. Neno la Mungu litatimia, kwa vyovyote vile. Inakubidi tu kusimama moja kwa moja kwenye Neno, na kusema, “Ni *hivi*,” na kulidumisha Neno. Sasa, angalia, kutengeneza kitu kupachukua mahali pa Neno Lake!

¹⁵⁹ Labda marafiki wa Ibrahimu, pia, kama tulipata kuona, labda marafiki wa Ibrahimu walipitia pale na kusema, “Vema, baba wa mataifa, una watoto wangapi sasa?” Wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja. “Aisee, baba wa mataifa, baba wa wengi, je! una watoto wangapi sasa?” Wenye kudhihaki!

¹⁶⁰ Sasa, hivi hamjauona ule wakati? Hivi hatujauona, wakati mara nyingine tumeombea jambo fulani, wala halikutukia?

¹⁶¹ “Huyu hapa mzee ameketi,” wanasema. “Yeye ni kipofu. Yeye ni kiziwi. Yeye ni bubu. Yeye ni mgonjwa. Amefanya jambo

hili. Nendeni pale mkamponye, enyi waponyaji wa Kiungu. Tutaliamini.”

¹⁶² Hivi wanatambua ni pepo yeye yule aliyesema, “Shuka msalabani, nami nitakuamini. Yageuze mawe haya yawe mkate, nami nitaamini”? Mnaona? Ibilisi yule yule aliyeyafunga macho ya Bwana wetu kitambaa, na kumpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Sasa, kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini.”

¹⁶³ Vema, mnajua Yeye alijua ni nani aliyempiga. Angaliweza kuyageuza mawe hayo yawe mkate. Ama, angaliweza kutoka msalabani. Lakini tungekuwa kitu gani leo hii kama angalifanya hivyo? Mnaona? Hawajui mpango wa Mungu. Huna budi kutafuta kujua kile Mungu ameahidi.

Sasa sina budi kuharakisha.

¹⁶⁴ Sasa, sasa huenda wangesema, “Baba wa mataifa, tulikusikia, miaka ishirini na mitano iliyopita, ukisema utampata mtoto kwa Sara, na kutokana na huyo mataifa ya watu yatatokea. Hivi una watoto wangapi wakati huu, baba wa mataifa?” A-ha! Mnaona? Hiyo ni maskini roho ile ile kinzani ambayo ingekosoa.

¹⁶⁵ Ibrahimu alifanya nini? Kasema, “Hakusita kwenye ile ahadi, kwa kutokuamini.”

“Mbona, hapa ulimwombea *Fulani*, wala hawakupona.”

¹⁶⁶ Hilo halijalishi. Kama nikiwaombea watu elfu kumi usiku wa leo, na elfu kumi wafe asubuhi, kesho usiku ningali ninawatia wagonjwa mafuta na kuwaombea. Mungu alisema hivyo. Halilikomeshi, hata kidogo. Mungu aliahidi hilo. Ninaliamini. Hakika. Haileti tofauti yoyote yale wanayosema, bado. Lakini, watadhihaki. Hiyo ni dhihaka ya Neno.

¹⁶⁷ Ibrahimu, akisimama juu ya Neno la Mungu, hatimaye lilitimizwa. Loo, jamani!

¹⁶⁸ Angalia dhihaka ya kuwa tasa. Akidhihakiwa, na dhihaka ya kuwa tasa, kwanza. Walikuwa na... Ilimbidi kuvumilia dhihaka ya kuwa tasa kwa miaka hiyo yote. Alikuwa na umri wa karibu miaka mia moja. Alikuwa na tisini, pamoja na Neno la Mungu lililosema ya kwamba yeye pia atakuwa ni *binti mfalme*, mama ya mtoto huyu. Na yeye ni tasa na Ibrahimu ni mgumba, miili ya—yao wote kama imekufa, bali hata hivyo kamwe hawakulitilia shaka Neno hilo, hata kidogo. Bali iliwabidi kustahimili hilo, kwanza. Halafu basi, haleluya, Mungu alilitimiza Neno Lake, katika saa hiyo yenye giza: Isaka alizaliwa. “Na uzao wake ni kama mchanga wa baharini ama nyota za Mbinguni.” Mnaona? Mungu daima hulijibu Neno Lake. Naam. Utasa kwanza, halafu Isaka.

¹⁶⁹ Zakaria na Elisabeti, vivyo hivyo, mzee huyo na mwanamke huyo mkongwe, bado wakishikilia. Na wakati Zakaria

alipopanda kwenda kule, naye angeweza kuandika kwenye kibao chake, na kusema, “Malaika alikutana na mimi, akaniambia ningemzaa mwana kwa Elisabeti, mke wangu mkongwe hapa. Siwezi kuzungumza tena. Mimi ni bubu. Nitakuwa bubu mpaka siku ambayo mtoto atazaliwa. Lakini mtoto yuaja, naye atakuwa ni nabii wa Aliye Juu Sana. Yeye ataitambulisha Nyota ya Asubuhi. Yeye ndiye mtangulizi wa Masihi.” Ingewezekanaje?

¹⁷⁰ Wengine walisema, “Maskini jamaa mzee. Loo, na—nadhani kidogo amerukwa na akili, unajua. Kuna kitu fulani kidogo. Lakini mwangalie maskini kizee Elisabeti pale, kwenye umri wa miaka themanini. Pia mwangalie—mwangalie—mwangalie Zakaria, mkongwe sana na anatemeka, na halafu atasema kitu kama hicho. Vema, maskini jamaa mzee huyo.”

¹⁷¹ Lakini alikuwa na Neno la Bwana. Dhihaka ya jinsi hiyo, hata huyo mke akajificha kwa siku kadhaa. Lakini mume alidumu na Neno. Loo, jamani!

¹⁷² Akikataa kupendwa na watu, akikataa maoni yanayopendwa na watu, akakataa tabaka la juu la siku hiyo, na mitindo na kadhalika ya siku yao. Waliikataa. Walikataa kutembea na umati wa wasioamini. Waliyakataa mambo ya ulimwengu. Iliwabidi kufanya jambo hilo, wapate kudumu na Neno la Mungu. Iliwabidi kufanya hivyo.

¹⁷³ Ndivyo ilivyo siku hizi. Unajitenga na kila kitu ila wewe na Mungu. Si yale kanisa linayofanya. Ni yale unayofanya na Mungu. Unaona? Ni wewe, kama mtu binafsi. Naam.

¹⁷⁴ Lakini angalia kile Mungu alichompa. Wakati Yesu Mwenyewe alipokuja, Zakaria alikuwa ameaga dunia. Elisabeti, pia. Lakini wakati mwana wao alipokuja nyikani, akiwa na BWANA ASEMA HIVI, Yesu alisema, “Hapajakuwapo na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kuliko yeye.” Amina. Nini? Yeye alipata dhihaka ya utasa. Alidumu katika Neno, naye akamzaa mwana kama huyo.

¹⁷⁵ Ni kama Sara wa kale, kama Ibrahimu wa kale, hao waume na wake wakongwe walilishikilia. Angalieni, wengi sana waliopata kuzaliwa, “kama mchanga wa bahari,” hakuna jamii ya watu ulimwenguni iliyo na watu wengi sana kama ya Wayahudi. “Kama mchanga wa bahari ama nyota za mbinguni.” Ni jambo gani lilikuwa limetukia? Lilitukia katika walio wachache, mtoto mmoja.

¹⁷⁶ Sasa mnaona mahali ninakoelekea. Mtoto mmoja, huyo tu ndiye aliyehitajika. Ilihitaji mtoto mmoja kuyatikisa mataifa na kumtambulisha Masihi. Ilimhitaji mmoja, mtiifu. Naam. Mungu anahitaji tu mtu mmoja. Huyo tu ndiye Yeye anayehitaji, mahali fulani anapoweza kupata sauti. Huyo tu ndiye anayemhitaji, kumpata mtu mmoja katika uongozi Wake. Loo, jinsi anavyopenda kumpata mtu mmoja!

177 Alimpata Nuhu, wakati mmoja. Alimpata nanii—alimpata Musa, wakati mmoja. Alimpata nanii—Yeremia. Alimpata nanii—Eliya. Alimpata Elisha. Alimpata Yohana. A—
anampata... Alimpata Samsoni. Mradi tu anaweza kumpata mtu mmoja wa kumwongoza, huyo ndiye Sauti Yake. Anaweza kuzungumza kupitia kwake. Anaweza kuukemea ulimwengu. Loo, jamani!

178 Jinsi anavyoonea njaa na kupanda, kumpata mtu chini ya mamlaka Yake, “Ambaye ninaweza kusema kupitia kwake. Ninaweza kuifanya Sauti Yangu ijulikane. Ingawa atastahimili dhihaka, bali nitaitambulisha Sauti Yangu.” Mnaona? Loo, naam.

179 Utasa, kwanza. Hana budi kuwa tupu, huna budi kuistahimili dhihaka ya utasa. Ilimbidi Sara kuistahimili. Vivyo hivyo Zakaria na Elisabeti iliwabidi kuistahimili.

180 Angalieni, siku hizi. Sasa nitasema jambo fulani. Angalieni siku hizi watoto wa yule kahaba. Ameyaweka mataifa chini ya utawala wa kisiasa wa madhehebu, yule kahaba na binti zake. Angalia ni kizazi cha jinsi gani cha madhehebu kilichoinuka, na jinsi wenye haki walivyo wachache. Msijali. Dumuni na Neno. Ni vyema.

181 Huenda ukadhihakiwa, ukaitwa mtakatifu anayejifingirisha. Huenda ukaitwa kila kitu, kila namna ya jina baya. Lakini, dumu papo hapo, ni Neno, dhihaka ya Neno, jambo watakalosema kukuhusu wewe.

182 Jamaa mdogo, huenda akawa hapa asubuhi ya leo. Yeye ni rafiki yangu; Jim Poole, kijana Jim, watu wa—wake. Aliulizwa hivi majuzi. Vema, alibatizwa hapa. Mtu fulani alimwambia, kasema, “Kama ulikuwa ubatizwe kanisani, kwa nini hukutafuta kanisa kubwa, kitu fulani?” Mnaona? Bali aliiona Nuru. Hivyo tu. Mnaona?

183 “Watoto wa wasio haki ni wengi kuliko walivyo wa wenye haki.” Naam. Vema. Jinsi walivyo wachache, wa wenye haki! Angalieni walivyokuwa ni wachache katika siku za Nuhu. Mnaona? Angalia walivyokuwa katika siku za Sodoma. Mnaona? Jinsi wenye haki walivyo wachache!

184 Ni watoto wangapi alio nao yule kahaba! Yeye anawazaa watoto kwa njia yoyote ya kale, bali wote ni watoto haramu. Kahaba huzaa kahaba. Mbwa humzaa mbwa.

185 Na Kristo humzaa aliyetiwa mafuta. Biblia humzaa mwenye haki, kwa hiyo hatuna budi kuvumilia wazo la kuwa kundi dogo. Ni jambo la neema jinsi gani!

186 Liangalie lile kanisa kuu la Efeso, kulikuwa na kumi na wawili tu ndani yake. Naam. Liangalie kundi tulilo nalo siku hizi, upande wao. Naam.

Kulikuwako na watu wanane tu katika siku za Nuhu.

¹⁸⁷ Kulikuwako na watano pekee katika siku za Lutu, la, wanne; Lutu na mkewe, binti zake wawili. Na mke aligeuka akawa nguzo ya jiwe baada ya kutoka, kwa kuangalia nyuma. Kwa kweli, watatu ndio waliotoka siku hiyo.

¹⁸⁸ Na Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku hizo.” Inatupasa tuangalie na kuwa waangalifu. Jinsi wenye haki walivyo wachache! Lakini, kama kawaida, wenye kudhihaki hawana budi kudhihaki. Ta-... Kuistahimili dhahaka ya utasa, kwanza. Jamani!

¹⁸⁹ Sina budi tu kuharakisha. Mimi ni...Sininii...Ninataka kusaidia kuwapata watoto hawa. Nivumilieni tu kidogo. Mnaona?

¹⁹⁰ Wanadamu daima ni wale wale tu. Sasa nitasema jambo fulani tena. Nami ninawatakeni...Wala sijui kama linarekodiwa, au la. Lakini kama liko kwenye kanda, ninawatakeni mnisikilize, ninyi mlio kwenye kanda. Msilikose, bali lichunguzeni. Mwanadamu sasa ni kama alivyowahi kuwa siku zote. Anamtukuza Mungu kwa yale aliyofanya; akitazamia mbele yale atakayofanya; na anapuuza yale amefanya na anayofanya. Yeye humsifu Mungu kwa yale aliyofanya; anatazamia yale atakayofanya; bali anapuuza yale Mungu anayofanya, na hapo anakosa kitu hicho chote. Natumaini wanakipata. Mnaona? Anapuuza yale anayofanya! Yeye anajua yale aliyofanya; naye anajua ahadi ya yale atakayofanya; bali anashindwa kuona yale anayofanya.

¹⁹¹ Loo, enyi Wapentekoste, kama ninyi sio mfano wa jambo hilo! Mnatazamia jambo fulani litukie: kama siku zote, lilitukia papo hapo chini yenu, wala hamjui. “Ni mara ngapi Yeye angewazunguka, kama kuku anavyowazunguka vifaranga wake, bali hamkutaka.” Mlifikiria zaidi juu ya mapokeo yenu na madhehebu yenu kuliko mliyolifikiria Neno Lake na Roho Wake. Naam.

¹⁹² Ni dhahaka ya jinsi gani kwa Mariamu! (Tunapofunga.) Ni dhahaka ya jinsi gani kwa Mariamu na Yusufu, kwa ajili ya Neno Lake. Ni wakati wa Krismasi. Nilikuwa nikipanga kushikilia kidogo tu, bali mtasikia mengi yake kwenye redio na miongoni mwa wachungaji, na kadhalika. Ni dhahaka ya jinsi gani kwa Mariamu na Yusufu, kushikilia Neno la Mungu la ahadi. Kumbukeni, sasa. Na dharau, huo mshangao mkubwa, walipomwona maskini Mariamu akipita, wakimwona Yusufu. “Unaoa malaya.” Mnaona? Pia kumbuka, ndugu, uzinzi ulikuwa ni mauti siku hizo. “Sasa, unamzuia asiuaawe. Yeye ana mimba yako.” Basi, ila, kumbukeni, wakati wote, Mungu alikuwa akiwashughulikia, na ilikuwa ni kulingana na Neno. Wala hawakujua jambo hilo. Mnaona?

¹⁹³ “Bikira atamzaa mtoto.” Yusufu alijua jambo hilo. Mariamu alijua jambo hilo, kwa sababu, baada ya Neno kuandikwa,

kulikuwako na Malaika akizungumza nao, akithibitisha, ama akidhihirisha Neno lile lile lililoandikwa, litakalotukia. Usiote ndoto sasa. Wazia. Roho Mtakatifu alishuka duniani; hakuzungumza na kusanyiko lote. Alisema nao.

¹⁹⁴ Yusufu aliangalia. Na kabla Malaika hajamtembelea, yeye alisema, “Vema, sasa, ninampenda. Lakini, mimi ni mtu mwenye haki. Siwezi kuoa mwanamke kama huyo.”

¹⁹⁵ Ndipo Malaika wa Bwana akamtokea, katika ndoto, na kusema, “Yusufu, wewe mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, kwa maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.” Loo, jamani! Ni faraja ya jinsi gani! Unaona?

¹⁹⁶ Na, Mariamu, akienda zake kisimani. Maskini bikira huyo, mwenye umri wa kama miaka kumi na saba, kumi na minane, akiolewa na mwanamume aliyekuwa ameo hapo awali na alikuwa na watoto wanne; mzee. Na msichana alikuwa... Alimpenda, wa—wala hakujua ni kwa nini. Na mwanamume huyu alimpenda msichana huyu, wala hakujua ni kwa nini. Nao hawa hapa, wakija, wakienda kisimani, kuchota maji. Na kutafakari kote juu ya mambo ambayo huyu msichana—huyu msichana alikuwa akiwazia, yale Maandiko, hapana shaka, na ndipo Nuru ikamulika mbele yake. Wakati Nuru hiyo ilipomulika, huyo hapo Malaika amesimama.

¹⁹⁷ Sijui maskini Mariamu alijisikiaje? Uliwahi kuwazia jambo hilo? Sijui kama alijisikia kufadhaishwa kama nilivyojisia jana.

¹⁹⁸ “Salamu, Mariamu!” *Salamu* maana yake ni “simama.” “Sikiliza kwa makini yale nitakayokwambia. Umebarikiwa miongoni mwa wanawake, kwa kuwa umepata kibali kwa Mungu, nawe utazaa Mtoto. Pasipo kumjua mwanamume, bali utamzaa Mtoto. Na binamu yako Elisabeti, akiwa mzee, pia, amepata mimba pia, naye atazaa mtoto. Na ishara hizi zitafanywa.”

Akasema, “Yatakuwaje maneno haya, kujua, kwa maana sijamjua mume?”

¹⁹⁹ Akasema, “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako. Kitu Hicho kitakachozaliwa kitaitwa Mwana wa Mungu.”

²⁰⁰ Acheni wenye kudhihaki waseme kile watakacho. Msichana alijua jambo hilo. Alijua litatukia, kwa maana Mungu alisema hivyo.

²⁰¹ Sasa, jinsi ambavyo hapana budi alijisikia, siku hiyo ya kuwekwa wakfu, ama walipokuja kwa ajili ya tohara ya Mtoto huyo, wakati alipokuwa akitembea hapo na Mtoto huyo mikononi mwake, namna *hiyo*. Na wanawake wote wakimwepa, wote wakiwa na nguo nzuri walizoshona, wakija kuwaweka wakfu watoto wao wachanga na kuwatahiri, na karibu hao wote wakimvuta mwana-kondoo. Lakini yeye alikuwa na hua wawili,

wa kusafishwa kwa utakaso wake. Maskini Mtoto huyo mchanga amefungwa kwa nguo za kitoto, zilizotengenezwa kutokana na nira iliyotolewa mgongoni mwa shingo ya maksai, nira, kifuniko cha mgongo wa maksai. Hizo zilikuwa tu ni nguo za kitoto horini. Hawakuwa na chochote kwa ajili Yake. Walikuwa ni maskini sana. Naye huyo hapa amesimama.

²⁰² Hapana shaka, wanawake wote walikaa mbali na maskini bikira huyo. Kasema, “Mnaona, yeye ana mtoto haramu.” Mnaona jinsi ambavyo Mungu hufanya mambo yaonekane ni ya kiwendawazimu sana. Loo, jamani! Yeye humpumbaza Shetani moja kwa moja. “Ni mchafu jinsi gani! Ni kinyaa jinsi gani! Uzinzi. Hivyo ndivyo huyo msichana alivyo. Yeye ni mzinzi.” Hilo halikusimamisha ule mdundo katika maskini moyo wa Mariamu. Walikaa mbali na Yeye.

²⁰³ Wangali wanafanya jambo lile lile, wanamwita sasa, “Mtakatifu anayejifingirisha, ama mlokole,” ama kitu fulani.

Mariamu alijua Huyu alikuwa ni Mtoto wa Nani. Aliendelea tu, vivyo hivyo.

²⁰⁴ Lakini, loo, si walipaswa kuona wakati, Simeoni, akiketi huko nyuma katika chumba hicho, alikuwa ameahidiwa? Alizunguka kila mahali, akitabiri. Akasema, “Bwana alinitokea.” Na akasema, “Sitaona mauti. . .” Naye alikuwa na umri wa miaka themanini na kitu wakati huo. “Sitaona mauti kabla sijauona wokovu Wake.”

²⁰⁵ “Loo, Simeoni, wewe ni mzee, mwanangu. Nanii wako—nanii wako. . . Mzee huyo kwa namna fulani amerukwa na akili, unajua, yeye kidogo. . . Mwache tu. Hana udhuru. Hatamduru mtu yeyote.”

²⁰⁶ Bali Simeoni alikuwa na Neno la Bwana, kasema, “Nilimwona Roho wa Mungu akishuka juu yangu. Nikasimama na kumwangalia. Yeye akaniambia, ‘Simeoni, umekuwa ni mtu mwenye haki. Na hutaninii. . . Nitakufanya ushuhuda huko nje.’” A—ha. Hivyo tu.

“Kwa nini Wewe ufanye jambo hilo, Bwana?”

“Hiyo ni kazi Yangu.”

²⁰⁷ Maoni yangu ni, ya kwamba hakika anaweza kuwamwagia kaa juu yao, kwenye Siku hiyo. “Mlikuwa na shahidi. Kwa nini hamkumsikiliza?”

²⁰⁸ Huyu hapo bikizee kipofu Ana, ameketi pale hekaluni, akiomba. Bwana alimfunulia, “Simeoni amesema kweli.” Amina. Asingeweza kuona nuru ya mchana kutoka gizani, bali angeweza kuona mbali zaidi kuliko wengi wa watu siku hizi walio na macho mazuri. Aliona, katika Roho, kule kuja kwa Masihi kulikuwa kumekaribia, Roho akitenda kazi moyoni mwake.

209 Mnaona jinsi lilikuwa ni Kanisa dogo sana? Zakaria, Elisabeti, Mariamu, Yohana, Ana, na Simeoni; sita kutoka katika mamilionni. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Sita wa hao. Mungu alimshughulikia kila mmoja wao. Wote walikuwa katika upatano. Wote walikusanyika pamoja. Amina.

210 Hapa, maskini mzee Simeoni. Huyu hapa maskini Mtoto Mchanga akaingia. Hakuwa amesikia jambo lolote kumhusu. Huyu hapa Mtoto huyo Mchanga. Na basi Simeoni aliketi chumbani mwake, na Roho akamshukia, kasema, “Toka nje, Simeoni.”

211 Huyu hapa anakwenda, akitembea, bila kujua mahali alipokuwa akienda. Kama vile Ibrahimu, alikuwa akitafuta kitu fulani. Hakujuua kilipokuwa, bali aliendelea kusonga mbele. Baada ya kitambo kidogo, akasimama. Na hapana shaka Roho Mtakatifu alimwambia, “Huyo hapo.”

212 Akanyosha mkono, katika mikono ya Mariamu, akamchukua Mtoto huyo Mchanga mikononi mwake. Akaangalia juu na kusema, “Bwana, mruhusu mtumishi Wako sasa aondoke kutoka katika maisha haya kwa amani. Macho yangu yanaangalia wokovu Wako.” Kitu kile ambacho kila mtu alikuwa akikidhihaki, kile wale wanawake walichokuwa wakikiepa, Simeoni alisema, “Ni wokovu Wako, Bwana.”

213 Na mnamo wakati huo, huyu hapa anakuja bikizee kipofu, akienda kwa kupapasa-papasa, akiyumbayumba katika halaiki. Ndipo akamjia, naye pia akatabiri, kwa maana alikuwa akimtazamia. Akamwambia Mariamu, “Upanga utauchoma moyo wako, bali utayatambua mawazo ya mioyo mingi.” Unaona? Ilikuwa ni kitu gani?

214 Sasa, nadhani, baadhi ya hao wanawake walisema, “Sasa angalieni jambo hilo! Mnaona ni tabaka la namna gani? Haya basi. Unaona? Jambo ndilo hilo. Mnaona mahali lilipo? Maskini mzee huyo, amepandwa na wazimu kichwani. Yule pale, amesimama mbele ya yule msichana malaya, akijaribu kusema kitu kama hicho. Haya basi. Huyu Mtoto haramu. Hebu mwangalieni maskini yule bikizee Ana, ameketi hapa, akijiua kwa njaa, na akiendelea namna hiyo. Hatapata burudani yoyote kama tuliyo nayo. Lakini, haya basi, mnaona. Angeweza kuwa mwanachama wa mashirika yote ya nchini hapa. Ametokana na familia nzuri sana, mnaona, naye angekuwa mshirika pale. Lakini huyo hapo. Mnaona jinsi kundi hilo linavyoambatana pamoja?” Loo, naam. Amina.

215 Ni jambo lile lile siku hizi. “Kuketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukiinuliwa juu na Roho Mtakatifu.” Hakika. Naam, bwana.

216 Loo, tuna wakati mwingine kidogo tu zaidi? Sina budi kusema jambo fulani. [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.]

217 Nina mtu mwingine hapa, ninayemwangalia, katika wakati huo ambapo Neno lilikuwa likidhihirishwa, wale mamajusi.

218 Laiti ningalikuwa na wakati, Fred, ili ulisome hilo. Unayo mfukoni mwako? [Ndugu Fred Sothmann anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nadhani wengi wenu mlilion kwenye gazeti.

219 Kitu ambacho Roho Mtakatifu alikizungumza hapa chini mtoni, miaka thelathini na mitatu iliyopita, walikifukua hivi karibuni tu. Desemba 9, wakikithibitisha, cha ule unajimu, jinsi ambavyo—ambavyo Jupita na hizo nyota, katika kundi lao!

220 Wana kale-...ya kale falaki, alama zake, waliifukua. Huo ndio wakati hasa kundi hili lilipoingia, katika kundi hili la nyota, nazo zikamulika moja kwa moja chini kuelekea Babeli, nao wale mamajusi wakazifuata. Mnakumbuka? Zilivuka mizingo yao, zikapembea chini, zimeachana kwa mabilioni ya miaka ya mwendo wa nuru tena. Na hao mamajusi wa Kiyahudi wenye hekima waliokuwa huko Babeli, waliliona kundi hilo likiingia kwenye kundi hilo, hizo nyota. Tatu za hizo zikakutana, pamoja, nazo zikafanyiza hiyo nyota moja ya asubuhi. Nao walijua jambo hilo kwa Neno la Mungu, kwamba huo ulikuwa ndio ule wakati, nyota hizo zinapokutana, kwamba Masihi alipaswa kuwa duniani.

221 Hiyo ndiyo sababu walianza, “Yuko wapi Yeye, aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Yuko wapi? Mahali fulani! Kwa maana, wakati nyota hizo zilipoingia, mpaka maumbo yao ya mbinguni yawe ni umbo moja kuu la mbinguni hapa, wakati hizo tatu zitakaposogea pamoja, Masihi atakuwa duniani wakati huo.” Basi wakati zilipoingia kwenye mizingo yao, hao watu walijua ya kwamba Masihi alikuwa duniani.

222 Walikuwa ni wataalamu katika fani yao. Walikuwa ni watu mashuhuri. Walikuwa ni wataalamu katika fani yao ya sayansi ya kidini. Walikuwa wakiangalia upande wa kidini wa jambo hilo. Nao waliziona hizo nyota zikisogea mbali kule angani, Jupita na Sargasi, na halafu zikaingia kwenye mstari wa—wao. Nao wakasema, “Tunajua ya kwamba Masihi yuko mahali fulani. Kwa hiyo, hapana budi Yeye yuko Yerusalemu, kwa maana hapo ndipo makao makuu ya dini ya ulimwengu, ya dini na Masihi. Hayo ndiyo makao yao makuu. Hayo ndiyo makao makuu ya kidhehebu. Hapo ndipo lile kundi kuu la kidini linapokutana.”

223 Nao hao wakaondoka kwa ngamia, miaka miwili, wakashuka kuvuka Mto Tigrisi, na kupitia kwenye vinamasi na misitu, wakisafiri, wakienda kwenye mji, mioyo imejaa furaha.

224 Walijua wakati hizo nyota zilipokuwa zikining’inia pale. Na hizi, hata wanajimu wanasema, siku hizi, “Kama kweli, hizo nyota, zikifika mahali hapo tena, zingefanya nyota moja, kutoka mahali walipokuwa wamesimama, wakiangalia.” Lakini

iliwabidi kuwa wamesimama kutoka mahali pale, wapate kuliona hilo. Amina. Amina.

225 Inategemea mahali unaposimama. Inategemea kile unachoangalia. A-ha. Naam.

226 Kwa hiyo waliiona, nao wakaifuata, nazo zilikuwa kabisa kwenye mstari. Haidhuru walifika wapi, zilikuwa moja kwa moja kwenye mstari pamoja nao. Iliwaongoza. Mnaona?

227 Hivyo ndivyo inavyokupasa kuyaunganisha Maandiko yote, kila kitu, kisha ukae mstarini pamoja na Maandiko. Hiyo ndiyo njia ya pekee. Itakuongoza moja kwa moja Kwake. Hakika itakuongoza.

228 Sasa angalia. Hawa hapa wanakuja, wakipaza sauti, “Yuko wapi, Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” Wakaingia Yerusalemu, ile Nyota ikawaongoza moja kwa moja kule, moja kwa moja kwenye makao makuu ya kidhehebu. Lakini walipogeuka waende kule, ile Nyota iliwaacha. Hao wakaingia mjini, huku na huku mtaani. Walidhani mji huo ungejaa furaha ya Mungu. Huku na huku mtaani, wakiwa na furaha, walienda, wakipiga makelele, “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliiona Nyota Yake tulipokuwa huko Mashariki, nasi tumekuja kumwabudu.”

229 Kumbukeni, ile Nyota, wao walielekea upande wa magharibi. Walikuwa Mashariki. “Wakielekezwa magharibi, wangali wakisonga mbele. Tuongoze kwenye...” Mnaona? Wao walikuwa kabisa... Walikuwa... Vema, Babeli na India ziko Mashariki mwa Palestina, kwa namna fulani kusini-mashariki. Nao walikuwa wakienda magharibi. “Wakielekezwa magharibi,” mnaujua wimbo huo, “wangali wakienda. Tuongoze kwenye hiyo Nuru kamilifu.” Mnaona? Hao, mamajusi walikuwa wakija magharibi. Wakiondoka Mashariki, wakielekea magharibi, nao wakaiona ile Nyota. Sasa, kama wanalikuwa Magharibi, wakiangalia nyuma, hawakuiona. Mnaona?

230 Wao, walipofika kule, iliwaongoza moja kwa moja kule, kisha ikawaacha. Nao wakawazia, “Hii hapa. Ile Nyota imeondoka, kwa hiyo jambo ndilo hili.” Wako mjini. Kwa hiyo, “Loo, jamani,” wakasema, “kila mtu anaimba tu na amefurahi. Utukufu wa Mungu umekiangazia kila kitu. Kwa hiyo, sisi hapa. Tunajua ya kwamba ninii yetu—tunajua ya kwamba ufanisi wetu, tulipokuwa tukiliangalia lile kundi la nyota, hakuna mtu, hakuna bwana, angaliweza kuja pale na kuziweka hizo nyota pamoja. Nasi tunajua, wakati hizo—wakati hizo nyota zitakapoingia kwenye sayari ya anga la juu, huo ndio wakati Masihi yuko duniani. Masihi yuko duniani.”

231 Na kila baada ya miaka mia kadhaa, zinapitia kwenye kundi lao tena, mnaona, ndipo kuna kipawa kinachokuja duniani. Angalieni.

232 “Masihi yuko duniani, wakati hilo—wakati kundi hilo la nyota linapoungana.” Nao walijua alikuwa hapo, kwa hiyo wakaenda kwenye makao makuu ya dini, na wakaanza kwenda, wakitangaza, huku na huku mtaani wakaenda, hawa ngamia, “Yuko wapi? Yuko wapi? Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliiona Nyota Yake Mashariki. Yuko hapa mahali fulani. Yuko wapi? Yuko wapi? Yuko wapi?” A-ha! Ni dhihaka jinsi gani!

233 Wakaenda kwa kuhani mkuu. Akasema, huenda alisema, “Mna shida gani ninyi watu? Inashangaza, enyi kundi la walokole!” Mnaona? Ni dhihaka jinsi gani, juu ya mafanikio yao ya kisayansi! Kwa nguvu za Mungu, waliiona Nyota Yake. Nao walikuwa ni mamajusi, werevu. Walikuwa kwenye fani ya sayansi ya kidini. Nao walijua, wakati hizo nyota zilipofika hapo, Masihi alikuwa yuko mahali fulani. Na hapa, mahali hapo ambapo walipaswa kujua jambo hilo, hawakuwa na habari.

234 Ningewazia, watoto walisimama mtaani, wakasema, “Angalieni kitu kile. Hao ni kundi la walokole. Wasikilizeni, wakiimba, ‘Yuko wapi, Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?’ Hawajui ya kwamba Herode ndiye mfalme mahali hapa. Hawajui askofu *Nanii*.” Loo, jamani!

235 “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliiona Nyota Yake Mashariki.”

236 Wao wanasema, “Njoni hapa, ninyi nyote mamajusi hapa, mliopo hapa.” A-ha. “Njoni hapa. Je! nyinyi nyote mnaona Nyota yoyote mahali popote?”

“Loo, sijaona kitu kama Hicho.”

237 “Ninyi wanafalaki nyote njoni hapa. Je! nyinyi nyote mliona nyota yoyote mahali popote?”

“La. La.”

“Je! mmeona kitu chochote kama ishara ya ajabu ya namna yoyote?”

“La. Hatuoni kitu kama hicho. La.”

238 Wala, hawakioni bado. Jambo lile lile. Hawaoni kitu. Hawawezi kukiona.

“En-he, hebu tuwaite ma—makasisi. Vipi ninyi nyote nanyi?”

“La. Kamwe hatujapata kuona Nyota yoyote.”

239 “Vema, vipi nanyi watu mnaolinda zamu, hapa nje ukutani? Mnaziangalia nyota. Mnajua mliwahi... Mnajua mahali kila kundi lililopo angani. Mnajua kila nyota. Je! mliona kitu chochote?”

“La. Hatujaona kitu.” Lakini ilikuwako.

240 Utukufu kwa Mungu! Loo, jamani! Hivi hamwezi kuliona Hilo? Liko hapo sasa, wala hawawezi kuliona. Linaendelea, papo hapo walipo, wala hawawezi kuliona.

241 “La. Hatukuona kitu. Loo, nilienda kule. Sikuona kitu.” Hakika. Huoni. U kipofu kupindukia. Si lako kuliona. Unaona? Kama wewe ni kipofu hivyo, mbona, hakika, hutalionia.

242 Ni kwa wale tu ambao Mungu atawafunulia. Hao ndio wanaoliona. Imekuwa hivyo daima. Hakika.

243 Nuhu ndiye angaliweza kuiona mvua angani, mwajua, bali hao wengine wasingeweza kuiona. Mnaona? Hawakuiona hiyo mvua huko juu, bali Nuhu anaiona.

244 Ibrahimu ndiye aliyemwona Sara amemshika mtoto mchanga. Hiyo ni kweli. Sio wenye kudhihaki ambao walisema, “Baba wa mataifa, una watoto wangapi sasa?”

245 Jinsi ambavyo tungaliendelea kupitia kwenye Biblia, wale wazee wenye hekima na manabii, kotekote! “Imani ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Wanajua Neno lililinena, nalo hilo hapo. *Huu* hapa ushahidi wake. Wanauona. Sasa angalia. Loo, jamani!

“Watu wetu wenye hekima hawaioni hiyo Nyota. Hakuna lolote.”

246 Kwa nini? Kwa kweli, wakati walipokuwa wakiangalia, nao wakaingia na kundi kama hilo, ile Nyota ilizimika.

247 Jambo lile lile siku hizi. Hilo ndilo linalozima Taa nyingi, hiyo ni kweli, ni kuungana na kundi kama hilo, ambalo hata haliamini jambo Hilo, kwanza kabisa. Basi tutakuwaje na mu—muungano wa makanisa? “Tutatembeaje pamoja tusipopatana?” Ni vipi ushirika wa . . . wa hili hapa, ulimwenguni kote, maninii yote—makanisa, makanisa yaliyoungana ya ulimwenguni? Tutaunganaje pamoja, wakati tumeachana kwa mamilioni ya maili? Unaona? Tutafanyaje jambo hilo? Wa Kiinjilisti pamoja nasi, na *hili*, na *lile*, na *lile*, na wote pamoja, na hata hivyo tumeungana na kundi kama hilo la upotovu.

248 Mungu anajitwalia Mke aliye safi, mtakatifu, asiyeghoshiwa, anayedumu na Neno Lake. Vema.

249 Dhihaka ya Yesu kwa Neno. (Ndipo tutakoma, mnamo dakika moja.) Yesu alidhihakiwa kwa ajili ya Neno. Angalieni hapa. Angeweza je kuistahimili dhihaka, wakati alipokuwa ni Mwenyezi, Mungu aliyefanyika mwili? Yeye alikuwa ni Mungu, Mwenyewe, aliyefanyika mwili.

250 Sasa, mnajua Biblia ilisema hivyo. “Tulimpapasa. Malaika walimwona.” Hebu wazieni tu jambo hilo. Ninaamini Timotheo analiweka kitu kama hicho. Mnaona? Ya kwamba, “Bila shaka siri ya uungu ni kuu; kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika.”

251 Malaika walikuwa mahali alipozaliwa. Jinsi ambavyo hapana shaka Malaika waliangalia chini na kushangilia, walipotazama chini kwenye hori na kumwona Mungu amefanyika mwili. Amina. Si ajabu walianza kupiga makelele,

“Leo, katika mji wa Daudi, amezaliwa Kristo Mwokozi.” Malaika walishangilia, nao wakayabembeza mabawa yao makubwa pamoja, na juu ya milima ya Yuda, wakaimba, “Utukufu kwa Mungu aliye juu sana, amani duniani, na kwa watu aliowaridhia.” Walilionga Neno la Mungu, ambalo walililinda, kuliona likidhihirishwa. Nalo lilikuwa ndilo hilo hapo.

²⁵² Sasa, Shetani hakuamini jambo hilo, mwajua. Yeye alisema, “Kama Wewe ni . . .”

Malaika akasema, “Yeye ndiye.” Hiyo ndiyo tofauti.

“Ikiwa wewe ni nanii, fanya *hivi na vile*. Hebu tuone Wewe ukilifanya.”

Bali Malaika alisema, “Yeye ndiye.”

²⁵³ Wale mamaajusi wakiwa na sayansi yao ya kidini, walisema, “Yeye yuko.” Amina.

²⁵⁴ Hiyo ndiyo sababu wataalamu wa elimukale na kadhalika siku hizi wanachimbua vitu hivi, ambavyo vimetabiriwa miaka michache iliyopita, ambavyo vingetimia. Nao hawa hapa, wakichimbua. Kamwe hata hawajaninii . . .

²⁵⁵ Hakuna historia iliyopata kusema ya kwamba Pontio Pilato alipata kuwa duniani. Hivi mlijua hilo? Baadhi yenu ninyi watoto wa shule niambieni ni wapi katika historia paliposema kuna Pontio Pilato. Nao wasioamini wanalidhihaki na kulifanyia mzaha, walisema, “Kamwe hapajapata kuwako na m—mtawala mkuu wa Kirumi aitwaye, ga—gavana aitwaye, Pontio Pilato.” Lakini karibu majuma sita yaliyopita, walichimbua jiwe la pembeni: Pontio Pilato, liwali. Loo, jamani! Upuuzi kama huo!

²⁵⁶ Walisema, “Kamwe hapajapata kuwapo na Ramesesi katika historia, Ramesesi juu ya Misri.” Lakini walichimbua jiwe, elimukale: Ramesesi, wa pili. Angalia.

²⁵⁷ Nao walisema ya kwamba hizo kuta kamwe hazikuanguka. Wanaakiolojia walikuwa wakichimba kule, na, muda si muda wajua, wakachimbua, huko chini kabisa ambako kuta zilianguka huko Yeriko, mwajua, wakati tarumbeta ililia. Wakasema, “Hiyo ilikuwa tu ni hadithi ya uongo, wimbo ambao mtu fulani alisema, aliimba huko nyuma.” Naam. Mwenye kudhihaki anasema hilo. “Hiyo ilikuwa tu ni hadithi ya uongo. Hapajapata kuwa na kitu kama kuta kuanguka, na Yoshua kupiga tarumbeta, na akakimbia hadi kwenye hizo kuta nazo zikaporomoka. Hakujapata kuwako na kitu kama hicho.” Ndipo mwanaakiolojia mashuhuri Mkristo akaendelea tu kuchimba, kwa kuwa alijua ilipaswa kuwa hivyo. Akachimba futi thelathini na kitu, chini ya mahali hayo mengine yalipokuwa. Hizo hapo kuta, zimelundikana mmoja juu ya mwingine, kama tu vile Neno lilivyosema.

258 Wakasema, “Hakukuwako na kitu kama Daudi akicheza ala yake, kinubi cha nyuzi, maana muziki wa nyuzi haukujulikana mpaka kwenye karne ya kumi na tano.” Wakasema, “Kamwe hukujapata kuwako na kitu kama hicho.” Wanaakiolojia Wakristo wakachimba, huko Misri. Miaka elfu nne iliyopita, walikuwa na ala za nyuzi. Amina. Loo, jamani!

259 Wao walisema, kuhusu wana wa Kiebrania kuyafanya yale mawe na vitu kama hivyo, kutoka kwenye majani, “Hakukuwako na kitu kama hicho.” Wanaakiolojia wakaanza kuchimba kule. Walipata nini? Hiyo ni sayansi. Walipata nini? Kuta za mji ambao Waebrania waliujenga, safu ya kwanza ya mawe ilikuwa ni majani marefu; ya pili ilikuwa imechongwa kwa vipande vidogo vya mashina ya mabua; nayo ya tatu haikuwa na majani ndani yake, hata kidogo. Loo, jamani!

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara wazizotabiri manabii.

260 Naam, bwana. Yote yamesonga mbele hadi wakati wetu, ndugu, dada. Ni kwa nini? Katika miaka michache iliyopita, ulimwengu wa sinema kamwe haujafanya yale umefanya. Kwenye skrini inakuja hadithi ya *Zile Amri Kumi* iliyohadithiwa na Cecil DeMille. Kwenye skrini hiyo yanakuja maisha ya Yesu Kristo kupitia kwa *Ben Hur*. Kwenye skrini inakuja *Yule Mvua Samaki Mashuhuri*, kuongoka kwa Petro. Na michezo hii yote ya dini, ambayo sinema zimeikataa, na kuichafua, na kuitupilia mbali. Lakini, Mungu, katika Nguvu Zake kuu, anazitangaza kote, haidhuru.

261 Sasa hivi, mambo hayo yaliyokuwa yamesemwa miaka michache iliyopita, mimi mwenyewe, maskini, mtumishi mdogo mnyenyekevu wa Mungu. Nilisema, “Ipo Nuru iliyosimama na kusema nami, na kuniambia mambo nitakayofanya.” Watu walicheka na kusema, “Kidogo amerukwa na akili.” Ile pale picha Yake. Sayansi iliipiga picha. Iko pale. Ni Kweli.

Nikasema, “Mwanamke huyo ametiwa uvuli wa mauti.”

262 Wao wakasema, “Mambo ya kivuli, sasa, huo ni upuuzi. Anayabuni tu hayo niani mwake.”

263 Hiyo hapo picha yake. Mungu atayafanya mawe yapige kelele. Yeye anaweza kufanya yale anayotaka kufanya.

264 Yesu, dhihaka kwa ajili ya Neno. Mwana wa Kiungu wa Mungu akisimama pale, Imanueli, ni dhihaka ya jinsi gani! Akamwacha mwenye dhambi asiyeamini kumfunga, kumtemea mate usoni Mwake, na kung’oa ndevu chache, na kumwacha athubutu kufanya lolote kuhusu hilo. Dhihaka kwa ajili ya Neno! A-ha. Ati nini? Kulitimiza Neno la Baba. Loo! Lakini, kumbukeni, Yeye hana budi kustahimili dhihaka ya mauti. Mungu, ambaye hawezi kufa, na Yeye pekee ambaye angeweza kufa apate kumwokoia mwenye dhambi. Hakuna mtu mwingine yeyote, hakuna nafsi ya pili ama nafsi ya

tatu, ingeliweza kufanya hivyo. Mungu Mwenyewe Ndiye tu anayeweza kulifanya. Na alikuwa ndiye Huyu hapa.

265 Alisema, “Hakuna mtu aliyepaa juu ila Yeye aliyeshuka chini, yaani Mwana wa Adamu aliye Mbinguni sasa.” Amina.

266 Wao walisema, “Baba zetu walikula mana nyikani.”

“Nao wamekufa,” akasema.

“Na ati unasema Wewe ni Mkate wa Uzima?”

267 Akasema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO. Mimi Ndimi Mkate wa Uzima. Ndimi MIMI NIKO.”

268 Wakasema, “Wewe hujapata bado miaka hamsini, nawe wasema kwamba ‘umemwona Ibrahimu?’”

269 Akasema, “Yeye Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Kisha akawaacha wenye dhambi kumfunga, kanisa la kimadhehebu, kumfunga.

270 Kumbukeni, katika siku za mwisho, kanisa hili tajiri la Laodikia, hata, lilimtoa nje, nje ya kanisa. Mnaona mahali lilipo sasa? Mnaweza kuona ni kwa nini ninaukemea mfumo huo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

271 Ni kwa nini Yesu aliwaacha wenye dhambi wamfunga? Ilikuwa ni kulitimiza Neno, kuleta dhihaka kwa Mungu, akifa. Ilimbidi Mungu kufa. Ilimbidi awe mwili, kusudi apate kufa. Naye Yesu alijua jambo hilo. Aliwaambia kuhusu hilo. Alisema, “Liharibuni hekalu hili, Nami nitalisimamisha tena.” Si mtu mwingine alisimamisha. “Nitalisimamisha. Katika siku tatu, nitalirejesha moja kwa moja tena. Ninyi liharibuni; nitalisimamisha. Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, kwa siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi.” Nao hata hawakuelewa na hilo. Mnaona? Dhihaka kwa ajili ya Neno, Yeye—Yeye alikuwa.

272 Sasa, alidhihakiwa hata kufa, apate kufufuka tena kwa Uzima wa Milele. Ilibidi kwanza auawe, kusudi aweze kufufuka kwa Uzima wa Milele, na kumleta kila mwanadamu mwingine (aliyekuwa katika umbo Lake) kwenye Uzima wa Milele, ambaye angeukubali. Unaona? Alifanyika mwanadamu, akawa Mkombozi wa jamaa yetu, na ikambidi kustahimili dhihaka zote za kudharauliwa kote, na kufanyiwa mzaha kote, kama tu watumishi wenzake walivyofanyiwa kabla Yake. Kama vile Musa, kama vile Nuhu, kama vile hao wengine wote walivyostahimili dhihaka hizo, ilimbidi kustahimili dhihaka. Kwa nini? Yeye alikuwa na Neno, Naye alikuwa ni Neno. Hiyo ndiyo sababu walimdhihaki zaidi ya yote ilivyowahi kuwa. Yeye alikuwa ni Mungu na ni Neno Lenyewe. Haleluya! Hilo ndilo lililomfanya Yeye.

273 Yesu alisema, “Enyi wanafiki.” Kasema, “Mnayajenga makaburi ya manabii, nanyi ndio mliowaweka mle ndani.

Walikuja na Neno la Mungu, wala hamkuwaamini. Ninyi mna hatia ya kila mmoja wao.”

²⁷⁴ Huko Phoenix, Mungu akipenda, nililipata neno hivi majuzi. Nitakishtaki kizazi hiki kwa kumwua Yesu Kristo, kumsulibisha upya. Nitaleta shtaka mbele ya shirika hilo la wahudumu, Mungu akipenda. Wana hatia ya Damu ya Yesu Kristo, kwa kumsulibisha upya. Naam, bwana. Kulishtaki lote!

²⁷⁵ Petro aliwashtaki, kwenye siku ya Pentekoste. Alisema, “Ninyi kwa mikono miovu mmemsulibisha Mkuu wa Uzima, ambaye Mungu alimfufua. Sisi tu mashahidi.” Yeye alileta shtaka.

²⁷⁶ Nitalichukua Neno la Mungu, nilishtaki kila dhehebu lililopo, na kila mtu aliye juu ya uso wa nchi, ambaye ana hatia ya Damu ya Yesu Kristo. Mungu na anisaidie niwe wakili Wake kwenye siku hiyo. Amina. Naam.

²⁷⁷ Loo, wenye kudhihaki walimdhihaki. Walimdhihaki. Yeye alidumu moja kwa moja Nalo. Amina. Loo! Angalia yale aliyofanya. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, alikufa kusudi aiangamize dhambi. Ilimbidi kufanya hivyo. Ninii . . . Hiyo ndiyo njia pekee ingaliweza kuangamizwa. Naye akaiangamiza na kuistahimili, maana hao wengine wote walikufa.

²⁷⁸ Kwa kuwa, wote hao huko nyuma walikuwa na Neno dogo la Mungu. Maana, Yesu alisema hivyo. “Ne—Neno la Bwana liliwajia manabii. Na ni nani kati yao,” Yeye alisema, “ambaye baba zenu, dini yenu ya kimadhehebu, hawakumpiga mawe na kumwua? Ni nani kati yao aliyewapokea manabii? Kisha mnajenga makaburi yao wakiisha kuondoka.” Kasema, “Ninyi mna hatia ya kuwaweka humo.”

²⁷⁹ Ndipo akawapa ule mfano kuhusu shamba la mizabibu lililokodishwa, nao watumishi wakaja. Wakawatenda mabaya, basi hatimaye wakasema, “Sasa tutamwua mwana, kwa kuwa yeye ndiye mrithi.” Mnaona? Loo, walikasirika walipolielewa hilo. Mnaona?

²⁸⁰ Lakini ilimbidi kustahimili dhihaka. Na hapa akaachilia afungwe, akaongozwa mautini, kusudi apate kuuawa, apate kuurudisha Uzima wa Milele. Utukufu kwa Mungu. Loo, jinsi ninavyompenda! Kuurudisha Uzima wa Milele na kumfufua kila mwana wa Mungu, kote katika wakati, ambaye alisimama na hilo Neno na akachukua dhihaka. Hiyo ni kweli.

²⁸¹ Kama asingalikuja, Nuhu asingalifufuka. Kama asingalikuja, Eliya asingalirudi. Kama hakuja, Nuhu asingalifufuka kamwe, kama . . . asingeninii, kama asingalikuja. Maana, Yeye alikuwa ndiye yule Mwana-Kondoo aliyechaguliwa tangu zamani, aliyekuja kuchukua dhihaka juu ya nafsi Yake, na apate kulifia kila Neno la Mungu lililokuwa limenenwa, na ambalo hawa watu wenye haki wameshindania. Ilimbidi kufa. Hakuna mwingine angeweza kufa. Mungu Mwenyewe, Naye

alikuja na kupachukua mahali hapo, kusudi apate kumkomboa na kumpa Uzima wa Milele kila mwana wa Mungu ambaye amelishindania Neno lile lile na angepata dhihaka. Kila mwana wa Mungu, kote katika wakati, ambaye angestahimili dhihaka, hakuna mtu angaliweza kumkomboa, bali kwa imani yeye alimwona huyo Mkombozi akija.

²⁸² Ayubu alimwona. Ayubu alisimama huko nyuma, nao wakasema, “Loo, wewe ni mwenye dhambi wa kisiri. Mungu anakutesa tu, maana wewe ni mwenye dhambi wa kisiri.”

²⁸³ Akasema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai. Katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yatauharibu mwili huu, hata hivyo, katika mwili wangu nitamwona Mungu.”

²⁸⁴ Mkewe akasema, “Mbona usimkufuru ukafe?” Kasema, “Unaonekana kama fukara mwenye mashaka sana.”

²⁸⁵ Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu.” Amina. Alikuwa ndiye huyo hapo. “Ninajua Yeye yu hai, Naye atasimama katika Siku ya mwisho.”

²⁸⁶ Kama Yesu asingalikuja, Ayubu asingalikombolewa, maana Yeye alikuwa ndiye Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alijua mahali Pake. Alijua sehemu Yake.

²⁸⁷ Hiyo ndiyo sababu, Mariamu alitambua mahali hapo, ile siku ambayo alitoka huko. Alisema... “Kama mimi... Kama ungalikuya hapa, ndugu yangu asingalikufa.”

Yeye akasema, “Ndugu yako atafufuka tena.”

Akasema, “Naam, Bwana, katika ule ufufuo. Yeye alikuwa ni mvulana mzuri.”

Yesu akasema, “Lakini MIMI NDIMI huo ufufuo. Unaamini jambo hili?”

²⁸⁸ Akasema, “Ndiyo, Bwana, ninasadiki ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu Yule aliyekuwa aje ulimwengu.”

Akasema, “Mmemzika wapi?” Loo! Haya basi. Um-hum.

²⁸⁹ Yeye alitambua jambo hilo. Maskini mwanamke huyo hakuwa akisema jambo hilo. Alikuwa na pepo saba waliotolewa kwake. Yeye alijua nguvu za Mungu, ambazo zingeweza kuondoa majivuno na fadhaa na kila kitu, kutoka kwake, ambaye angeondoa maskini roho hiyo choyo ya sekondari ya juu kutoka kwake, na ingemfanya kiumbe kipa. Alitoa pepo saba. Hao wanawake walijua kile Yeye alichokuwa, waliomkubali.

²⁹⁰ Walijua kile angaliweza kuwatendea. Vivyo hivyo wao wanajua siku hizi, pia. Likubali tu. Hilo ndilo jambo linalofuata.

²⁹¹ Huyo hapo. Yeye alisema jambo hilo. Naye alininii... Mnajua kile kilichotukia. Loo!

²⁹² Wote ambao wangeteseka kwa ajili ya Neno lilo hilo, Yeye alikufa kwa ajili ya jambo hilo. Yeye Ndiye tu angaliweza kufa, kufanya jambo hilo, kwa kuwa alikuwa ni Neno. Yeye alikuwa ni Neno, Neno lililodhihirishwa. Hao wengine wote walikuwa na kasoro kidogo, bali hapa palikuwapo na utimilifu wa Mungu, ndani Yake. Vivyo hivyo ndivyo alivyo leo. Waebrania 13:8, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Sikilizeni.

²⁹³ Ninafunga, kweli. Nitafunga, sina budi kufunga. Nimepita wakati wangu kwa mbali.

²⁹⁴ Kamwe hakuandika Neno moja. Je! aliandika? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Hakuandika hata moja. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno. Yeye alikuwa nini? Maneno yaliyokuwa yameandikwa, Yeye alikuwa ni dhihirisho la Neno hilo. Utukufu! Whiu! Sasa ninajisikia vizuri. Yeye alikuwa ni Neno. Haikumbidi kuandika chochote. Yeye alikuwa ni Neno, Neno Lake lililoandikwa, lililodhihirishwa. Utukufu kwa Mungu! Ni yeye yule leo, jana, leo na hata milele. Yeye ni Neno, Neno lililodhihirishwa.

Mnasema, “Je! hiyo ni kweli, Ndugu Branham?”

²⁹⁵ Mwangelie Yehova akisimama kule nyuma na kupulizia mchirizi kupitia kwa hayo yanayoonekana kama mawimbi kule, na akawatengenezea Israeli barabara wapitie.

²⁹⁶ Mwangelie Yehova katika mwili, akisema, “Amani, tulia.” Wakati mawimbi yalipokuwa yakipiga ufukoni, katika dhoruba, na shetani akipiga kila kitu, namna hiyo, Yeye akasema, “Amani, tulia.” Nayo ikamtii; hizo pepo na kila kitu. Yeye alikuwa ni Yehova. Amina.

²⁹⁷ Huyu Yehova ambaye angaliweza kusimama kule na kunyunyizia matone machache ya umande, akayaacha yaanguke ardhini na yawe mkate, kuwalisha watu.

²⁹⁸ Yeye alisimama na kuwachukua samaki watano, ama, mikate mitano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano.

²⁹⁹ Yeye alikuwa ni Neno. Amina. Amina. Yeye ni Neno, Naye daima atakuwa Neno. Na kwangu mimi na nyumba yangu, tatalitumikia Neno.

Loo, ninataka kumwona, nataka kuuangalia
uso Wake,
Hapo nikaimbe milele kuhusu neema Yake
iokoayo;
Katika mitaa ya Utukufuni, jalia niiinue sauti
yangu;
Wakati shughuli zote zimekwisha, na hatimaye
niko nyumbani, nikafurahi daima.

³⁰⁰ Loo, jamani! Naam. Kuchukua dhihaka ya Neno. Kuna dhihaka inayoambatana na Neno. Dumu moja kwa moja na Neno, na uistahimili dhihaka.

Na tuombe.

³⁰¹ Yesu, kama hivi majuzi usiku, Bwana, nilivyolia “Ee Yesu, ungetaka nifanye nini? Nifanyeje, Bwana? Nikiyaona mambo haya, na kujua saa tunayoishi, nifanyeje, Bwana? Nifanyeje?”

³⁰² Ninaliombea kanisa langu dogo hapa, Bwana. Ninawaza juu ya wale ndege wadogo kwenye lile ono, mambo ambayo yamekuwapo; na hao ndege wengine, ambayo yalikuwa ni mambo makubwa. Lakini kulikuwako na safu tatu zao, Bwana. Lakini wakati hao Malaika walipoingia, hapakuwapo na ndege waliosalia. Hao wajumbe wadogo wamekuwa ni wazuri sana, Bwana, bali ninaamini kuna jambo fulani lililo tayari kutukia. Na liwe, Bwana. Tufinyange na utufanye kulingana na njia Yako. Sisi ni—sisi ni udongo wa mfinyanzi. Wewe Ndiwe Mfinyanzi.

³⁰³ Kwenye mkesho huu wa Krismasi, Bwana, tunashukuru kwa ajili ya kipawa cha Mungu, kwa Mungu kutupa. Ingawa huu ni baadhi yake, kama tunavyoamini mioyoni mwetu, ushirikina fulani wa kikafiri wa siku ambayo wamejaribu kuitengeneza na kuifanya iwe kama mi—misa, misa ya Kristo, lakini sisi hatuji katika njia hiyo ya Baba Krismasi na miti ya Krismasi na—na mapambo. Bali tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, kumwabudu Mungu wa Mbinguni, aliyefanyika mwili, mwili kama sisi, na akakaa miongoni mwetu, apate kutukombo; na akapata dhahaka ya lile Jina, akapata dhahaka ya msalaba, akairuhusu taasisi ya kilimwengu kumwua Imanueli, kusudi Yeye aweze kutuletea Uzima wa Milele.

³⁰⁴ Sisi ni akina nani, Bwana? Tu nani sisi, kwamba tuepe dhahaka yoyote? Mungu, tufanye askari shujaa. Ninayakabidhi maneno haya Kwako, Baba. Huenda yamevunjika-vunjika; nikiwa nimechoka na kudhoofika hivi. Lakini, Baba, watuze watu hawa kwa ajili ya kuketi na kusikiliza. Na jalia nguvu zilizomleta Bwana wetu, na kutupelekea sisi hapa kama Mwokozi, katika siku hizi za mwisho, jalia ziihushie kila roho hapa, Bwana, kwa ajili ya kukaribia kwa kule Kuja kwa Bwana Yesu. Jalia iwe hivyo, Baba.

³⁰⁵ Waponye wagonjwa na wanaoteseka walio miongoni mwetu. Ifunge mioyo iliyovunjika. Bwana, sisi. . . Tumepitia mengi sana, moyo wangu una kovu nyingi sana juu yake, Bwana, kutoka kwenye vita vikali. Mimi ni askari mkongwe. Nisaidie, Bwana. Ninahitaji msaada Wako. Labda mafunzo haya yote yamekuwa ni kwa kusudi fulani. Ninatumaini yamekuwa hivyo, Bwana. Nisaidie, Ee Mungu. Na ulisaidie kanisa hili. Na utubariki, pamoja.

³⁰⁶ Wabariki watoto hawa wadogo. Ninawazia juu ya wengi leo, wadogo, maskini jamaa wadogo, ambao hawatapokea chochote huko nje. Nami ni—ninaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao na kuwasaidia. Wape Uzima wa Milele, Bwana. Huo ndio mkuu. Hiyo ndiyo Zawadi ya Krismasi tunayotaka, ni

Uzima wa Yesu Kristo kutawala na kumiliki moyoni mwangu. Hivyo ndivyo ninavyotaka, Bwana.

³⁰⁷ Tubariki, pamoja sasa. Tunayakabidhi Maneno haya Kwako. Jalia yaanguke popote yatakapoanguka, Bwana. Popote ambapo mioyo itafunguka, jalia yalete wakati mkuu wa wokovu, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁰⁸ Yeyote ambaye...Ni wangapi wanaompenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kwa nini kuwa na haraka jinsi hiyo, kwa vyovyote vile? Loo, ninampenda! Ninampenda. “Bwana, wataka nifanye nini?”

³⁰⁹ Msizisahau ibada usiku wa leo. Mnajua maana ya Krismasi sasa? Loo, *Hii* ndiyo zawadi yangu ya Krismasi. *Hili* ndilo lile Neno. Bwana, kama ninaweza tu kujiachilia, kama ninaweza tu kujiiondoa njiani kusudi Neno Lako liweze kujidhihirisha, Lenyewe kupitia *hapa*, hilo ndilo—hilo ndilo jambo kuu sana nilijualo.

³¹⁰ Sasa nafikiri wana vitu fulani wanavyotaka kuwapa watoto. Sasa nitairudisha ibada kwa Ndugu Neville. Mungu awabariki.

Ndugu Neville.



DHIHAKA KWA SABABU YA NENO SWA62-1223

(The Reproach For The Cause Of The Word)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 23 Desemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org